RWANDA

HALI YA NCHI 2021

ILANI HURU YA KULETA PAMOJA, KUPONYA, KUTUNZA USTAWI NA KUIWEKA RWANDA INAYOSHAMIRI KWENYE TAIFA LA AFRIKA MASHARIKI

Theogene Rudasingwa

Eugene Ndahayo

Nkiko Nsengimana

Joseph Ngarambe

Sixbert Musangamfura

Jonathan Musonera

UTANGULIZI

Ni msimu usiyoridhisha, unaofanana na hali ya utekaji nyara. Muonekano wa utulivu wa kuhadaa, mitaa yenye unadhifu, hali ya utulivu ifichayo hasira, karaha, huzuni, hofu, kukosa matumaini na majonzi yasiyoelezeka. Rwanda imo tena kwenye mvutano mkubwa usio wa kawaida, uliyonaswa katika hali ya kuwa tayari kimapambano na sintofahamu ambayo imepelekea ukatili na simanzi isiyokoma.

Matukio ya mwaka 2020 na ile miezi ya awali ya mwaka 2021 yanasomeka kama marudio ya kiama yaliyochanganyikana na vichekesho. Janga la Virusi vya Korona 2019 vimeweka zuio juu ya zuio linguine la kutokutoka nje nchini Rwanda. Nchi yenyewe ilikwisha kujifungia yenyewe kwakuwa mipaka ya Rwanda-Burundi, Rwanda-Uganda ilikwisha kufungwa, wanachi wa Rwanda wamefungiwa katika hali ya muendelezo wa kufungiwa ndani, na kila mtu huru akizuiliwa na kanuni za majeshi ya ndani chini ya polisi wa siri wa jenerali Kagame, wauaji DMI.

Orodha ndefu inazidi kuongezeka ya wahanga wa Rwanda kwenye mikono jeuri iendelezayo majanga. Mpendwa Kizito Mihigo na muimbaji maarufu, mtusi na manusura wa mauaji ya kimbari alikutwa ameuawa gerezani. Kwa kuimba na kuhubiri upatanisho wa dhati unayojali na kukumbatia wahanga ambao ni Wahutu na Watusi alikuwa ameukosea mtazamo wa maofisa wa utawala wa kuwa watusi ni wahanga na wahutu ndiyo waliofanya mauaji ya kimbari.

Paul Rusesabagina, mhutu aliyejipatia umaarufu katika filamu ya “Hoteli Rwanda”, aliwekewa mtego na polisi wa siri huko Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu na kujikuta Kigali amefungwa pingu alipokuwa akishuka kutoka kwenye mojawapo ya ndege binafsi anazozimiliki jenerali Kagame. Rusesabagina ameshitakiwa kwa makosa ya ugaidi, hati ya mashitaka ifananayo na blanketi ambayo husomewa yeyote yule anayethubutu kusema dhidi ya udhalimu na udikteta nchini Rwanda.

Manusura mwingine mtusi, Yvonne Idamange aliwekwa chini ya ulinzi na kushitakiwa kwa kosa la kubambikiwa la kuhatarisha usalama. Nchini kwa sasa, wanyarwanda wanatazama pasipokuamini vichekesho na uongo wa mashtaka ya washirika wa jeshi la msituni lililokamatwa nchini Kongo, wakituhumiwa kwa kosa la ugaidi. Kama hii haileti chukizo kiasi cha kutosha, utawala huweka kwenye mitandao ya kijamii maonyesho ya viungo vilivyotenganishwa vya miili ya viongozi wa waasi.

Kuna vichekesho pia, katika ukawaida wake wa kutaka makubwa jenerali Kagame husafiri kwenda Paris, Ufaransa akiwa na ripoti mbli za kigeni. Moja, Ripoti ya Ufaransa (*Ripoti ya Duklert* iliyoandaliwa na kamisheni iliyoongozwa na Mwanahistoria wa Ufaransa aitwaye Vincent Duclert) na nyingine kutoka kwa wamarekani (*Ripoti ya Muse* iliyoandaliwa na Joshua Levy na Robert Muse) izungumziayo kuhusika kwa Ufaransa katika mauaji ya Kimbari ya Rwanda

pasipo kusema chochote kuhusiana na rekodi ya matendo ya Paul Kagame. Ripoti zote mbili ni dhahiri zipo kimya juu ya ushiriki wake katika kuwaua marais Habyarimana na Ntayamira, ramani ya Umoja wa Mataifa (UN) ya mwaka 2010 yenye kuonyesha wapi msaada ulitokea, wapi tukio lilifanyika na uhisiano baina ya wahusika, uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu, mauaji ya kimbari ya wahutu nchini Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Michela Wrong, mwandishi wa habari uingereza alipochapisha kitabu kiitwacho *Do not Disturb "Usisumbue"* kinachoelezea uchunguzi sahihi wa utawala wa jenerali Kagame, jeshi lake na …… walivurumisha tuhuma nzito za kibaguzi dhidi yake.

Kwa kupoteza tumaini, wanyarwanda wengi husambaza uvumi, dhidi ya uhalisia ya kwamba jenerali Kagame amefariki. Ni ukweli upi juu ya hali ya mambo nchini Rwanda? Kuna uhalisia gani unaoweza kuhusishwa na matukio haya tofauti tofauti? Ni ukweli upi umejificha nyuma ya mitaa safi, maghorofa marefu yenye kuvutia ya hoteli za hadhi ya nyota tano na mali nyinginezo.

HISTORIA KWA UFUPI (1894-2021)

Uvamizi wa wakoloni wa kijerumani wa karne ya 19 ulitokea kipindi ambacho ufalme ulikuwa ukipitia mabadiliko ya kitawala kama matokeo ya kugombania madaraka miongoni mwa koo za kifalme za watusi. Ijapokuwa kwa karne nyingi Rwanda imetawaliwa na wafalme watusi, kubadilika kwa vurugu za matukio ilielezwa na wanahistoria kama mapinduzi ya Rucunshu (1896) yalikuwa alama ya wakati muhimu ulioamua namna gani nguvu za kisiasa zingepatikana, kulindwa na kupotezwa katika karne huko mbeleni. Kupitia muingiliano wa hadithi zisizo za kweli, mashirika ya kijeshi, mipangilio ya kijamii na kiuchumi, Rwanda ina jamii ya mpangilio wenye ufalme kamili juu kabisa na wengine wote chini yake. Siyo kila watawaliwa walikuwa na hadhi sawa mbele ya mtawala. Kwa ufupi ni kuwa, watwa walikuwa chini kabisa ya mfumo huo wa kijamii na kiuchumi huku wahutu wakifuatia na wingi wao na watusi kwa uchache wao wakiwa juu kabisa.

Hii ni asili na maendeleo ya utawala wa kifalme wa Rwanda uliorahisishwa na wenye kueleweka. Ugumu wa maingiliano ya mahusiano yalihusisha uvamizi wa kijeshi, mabadilishano yenye maridhiano pande mbili, uhusiano wa mabadilishano ya vitu baina ya watu wa jamii moja na nyingine (ubuhake), ambako mifugo ilitumika sana kama kiunganishi na tabaka la machifu (ardhi, mifugo na jeshi) waliosimamia milki za mfamle kwenye himaya yake. Washirika wa watunga mashairi (Abasizi) walipandisha madaraka ya mfalme, watafsiri wa mifumo (Abiru), hawa walihakikisha mpangilio wa urithi wa madaraka na kuvutia kwa kiwango cha hali juu

mbele ya mahakama ya mfalme haya yalijirudia kwa karne nyingi. Hata wakati ule, wafalme wa Rwanda hawakuwahi kutawala kikamilifu himaya yote ambayo ni Rwanda ya sasa. Hiki kiliwezekana kwa mfalme Musinga kwenye Rwanda nyingine kwa msaada wa wakoloni wa kijerumani mwanzoni mwa karne ya 20. Mipaka ya mashariki ya Rwanda ikijulikana kama Gisaka wakati ule, ilikuwa imetawaliwa kikamilifu na mfalme Rwogera wa karne ya 19 aliyetawala kabla ya mvamizi wa falme aliyeogopwa, mfalme Rwabugiri wa katikati ya karne ya 19. Ni kufuatia kifo cha mfalme Rwabugiri ndio kikatengeneza mazingira ya mapinduzi ya mfalme Rucunshu ambapo mrithi stahiki wa kiti hicho, mfalme Rutalindwa aliuwawa. Malikia maarufu aliyekuwa katili na mtu wa njama ovu, Malikia mama Kanjogera alimpindua mwanae mfalme Yuhi Musinga, baadaye kijana mdogo akitawala kwa usaidizi wa wajomba zake Kabare na Ruhinankiko.

Awamu ya kwanza 1: Utawala wa kijerumani (1894-1916): Ni katika fukuto hili maofisa wa jeshi la Ujerumani linatokea eneo la Rwanda, wanaweka utawala wa kijerumani juu ya utawala wa mfalme wa Rwanda. Milki ya Rwanda ikawa chini ya koloni la Ujerumani la Afrika Mashariki ambalo lilijumuisha na Tanganyika. Wazungu waliyoigawa Afrika miongoni mwao kwenye mkutano wa Berlini kati ya mwaka 1884-1885 walifahamu juu ya uvamizi wa kijeshi, haki ya utawala, urithi wa kifalme, utawala wa kiimla, utawala unaomilikiwa na wachache, ujima na ubaguzi. Waliunda kila kitu. Jamii zao zilikuwa zimepangiliwa hivi. Japo Rwanda ilikuwa ngumu na kuzidi uelewa wa maofisa wa kijerumani, bado waliweza kuweka utawala uliosawa ambao ungewapa udhibiti na utawala wa kikoloni.

Walizielewa pia hadithi ambazo zilizungumzia nguvu za mfalme wa Rwanda. Ukuu wa watusi, nguvu za kifalme, utawala wa kimungu uliorithishwa.

Kwa ajili ya matakwa yao ya kisiasa, shughuli za utawala wa kikoloni, mara baada ya kuanzishwa zilimsaidia Mfalme Musinga kuwatawala maadui zake hasa uhuru wa jamii za Wautu.

Awamu ya 2: Utawala ya Kibelgiji (1916-1962: Utawala wa Kijerumani ulidumu kwa muda mfupi, haukuwa na madhara makubwa kwa Ubelgiji mara baada ya kuchukua nafasi. Kama wajerumani kabla yao, uendeshaji wao ulianzia kwenye hatua ya usimikaji wa utawala wao kwa uvamizi wa kijeshi, kuweka tabaka juu ya uongozi wa kifalme uliopo. Mfalme, machifu wake na wote walioko chini wangeweza kwa ufanisi kuwa chini ya utawala wa mfalme wa Ubelgiji, wakiwakilishwa na gavana mtawala. Kanisa Katoliki, uanzishwaji wa elimu ya kimagharibi, usimamizi wa nguvukazi zilizopatikana kwa nguvu nchini Rwanda ulikuwa na madhara makubwa katika mageuzi ya ukoloni na utawala wa kifalme nchi Rwanda. Mfalme Musinga alikuwa ni mmojawapo wa wahanga wa mapema wa upepo kubadilika ambao ulikuwa unavuma juu ya vilima vya Rwanda. Hatimaye alikuja kupotezewa na Kanisa Katoliki, kutupiliwa mbali na

utawala wa kikoloki mnamo mwaka 1931 na akafia uamishoni. Alirithiwa na mwanaye aitwaje Mfalme Mutara Rudahigwa.

Japokuwa elimu ya kimagharibi ilikuwa kimsingi ni ya machifu wa kitusi ili kuhudumu kama makarani, watafsiri na watoza ushuru kwenye utawala wa kikoloni, seminari za Kanisa Katoliki zinakuaja baadaye kuenea kwenye idadi ndogo ya wahutu, hivyo basi kutoa sababu ya msingi ya uundwaji wa Kujitambua kwa wahutu ambako ukapelekea mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959. Usimamizi wa kulazimisha watu kufanya ndani ya Rwanda (uburetwa) kwa kiasi uliwakomboa wahutu kutoka kwa wafalme wa kitusi na ukakoleza muendelezo wa malalamiko ya msingi yaliyokuwa yamejilimbikiza kwa muda mrefu wa karne na karne. Hili pamoja na sera ya Ubelgiji ya kuwagawa wanyaranda kulingana na idadi ya umiliki wa mifugo na sifa za kimwili zilizidisha utambulisho wa kikabila, utofauti wa kikabila kwa wenye nacho na wasio nacho na kuongezeka kwa ukatili ambao ulikuja kuwa sifa ya msingi sana ya ubishano wa kisiasa nchini Rwanda. Kwenye kipindi cha baada ya vita ya pili ya dunia, waafrika waliongezeka wakitaka kujiweka huru kutoka kwa wakoloni wa kizungu. Ndani ya Rwanda, kipindi hiki kiliambatana na utawala wa kikoloi na Kanisa Katoliki hatua kwa hatua wakibadilishana nafasi na kuunga mkono makundi ya waseminari waliokuwa wakitaka kukombolewa kwa wahutu mara ya kwanza na mwishowe utawala wa kikoloni. Gregoire Kabiyanda aliongoza kundi huku akiunda chama cha siasa cha MDR-PARMEHUTU. Kwa upande wao wanaufalme, UNAR kilichokuwa kikitaka ukomeshwaji wa utawala wa kikoloni na uendelezaji wa kawaida yao.

Hatua hii ilikoma baada ya kifo cha ghafla cha Mfalme Mutara Rudahigwa kule Bujumbura, Burundi, katika mazingira ya kutatanisha ambayo hayakuwahi kuchunguzwa mpaka sasa. Na nchi ilivyokuwa inazidi kudidimia kwenye machafuko na mapambano yakianza, Kigeli Ndahindurwa, alifanywa kuwa Mfalme mpya wa Rwanda.

Awamu ya 3: Uasi wa kihutu wa 1959 (1959-1962): Ubaguzi na utengano wa kikabila uliongezeka sana pale UNAR na MDR-PARMEHUTU walipopigania ukuu, wakati Kanisa Katoliki na utawala wa kikoloni wa Ubelgiji kwa uwazi na kwa nguvu wakisimama upande wa wahutu. Pale taifa lilipotumbukia kwenye machafuko yaliyotumika na pande zote mbili, MDR-PARMEHUTU walishinda mapambano kwa namna ambayo kwa sasa inajulikana kama mapinduzi ya Gitamara ambapo tawala kongwe za kifalme za nchini Rwanda zilivunjwa na taifa likatangazwa jamhuri mnamo tarehe 28 Januari 1961. Dominique Mbonyumutwa akatawazwa rais wa mpito wa Rwanda na Gregoire Kayibanda akawa waziri mkuu.

Akiwa safari kuelekea Burundi, Mfalme Kigeli Ndahindurwa alizuiliwa kurundi nchini Rwanda na utawala wa kikoloni wa Ubelgij, alisalia uhamishoni kwa muda miongo mingine mitano mpaka mauti yalipomkuta huko nchini Marekani tarehe 16, oktoba 2016. Kipindi hiki kilishuhudia kuibuka kwa uvamizi wa kijeshi kutoka kwa nchi jirani na waasi wa kitusi chini ya jina la *Inyenzi,*

kupelekea mawimbi ya wakimbizi na mashambulizi ya visasi na mauaji ya kimkakati dhidi ya watusi kutoka kwa wahutu.

Wakati wa kipindi hiki, tukio linalokumbukwa sana nim pale ambapo utawala wa kifalme wa watusi ulipoanguka na tabaka la juu la watusi kutupiliwa mbali, washindi hawakujali juu ya watusi wa hali ya chini ambao waliuwawa maelfu kwa maelfu kwa kile kilichodaiwa kuwa kama mauaji ya kimkakati na baadhi yao, kama mauaji ya kimbari na iliyokuwa Vatikani kwa wakati ule. Hivyo, kutokea hapo kukawepo na mamia ya maelfu ya wakimbizi watusi kila pande za Afrika mashariki na kati na dunia kwa ujumla.

Tarehe 1 Julai 1962, Rwanda ikajitangazia uhuru wake kutoka kwa Ubelgiji na Georgie Kayibanda akawa rais wa jamhuri.

Awamu ya 4: Jamhuri ya Kwanza (1962-1973): Chini ya rais Georgie Kayibanda, Rwanda ilikuwa taifa la chama kimoja, hatua kwa hatua huku kukiwa na mfumo wa maamuzi kufanywa na mtu mmoja ambaye ni rais. Watusi waliosalia Rwanda wakawa na hadhi ya tabaka la kati. Tarehe 5 Julai 1973, rais Kayibanda akapinduliwa, katibu mkuu na waziri wa ulinzi meja jenerali Juvenal Habyarimana akaja kuwa rais mpya wa Rwanda.

Awamu ya 5: Utawala wa jeshi la kasjazini la wahutu (1973-1994): Chini ya utawala wake, meja jenerali Juvenal Habyarimana alizuia katiba na shughuli za kisiasa. Mwaka 1975 akaunda chama tawala pekee MRND, utawala wa kiimla mikononi mwake. Rais wa zamani Georgie Kayibanda akauwawa tarehe 15 Disemba 1976. Kuanzia 1974 mpaka 1977, takribani miaka 56 na pengine maelfu ya tabaka la juu kutoka kusini mwa Rwanda wakauwawa na kuzikwa kwenye makaburi yasiyojulikana. Kati yao walikuwa viongozi mashuhuri walioongoza mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959. Mateso ya watusi yaliendelea huku wahutu kutoka kusini mwa Rwanda wakatengwa. Mwaka 1979, Tanzania iliunga mkono waasi wa Rwanda kumpindua Idi Amin, na Umoja wa kitaifa wa muungano wa wanyarwanda ukaanzishwa na watusi nchini Uganda. Mwaka 1986, jeshi la msituni la Yoweri Kaguta Museveni (NRA) likakamata mamlaka ya utawala wa Uganda. Katika ngazi za vyeo za NRA wapo wakimbizi wa kitusi, mfano hai ni jenerali Gred Rwigyema. Mwaka 1987, chama cha mstari wa mbele cha kizalendo (RPF) kikazaliwa nchini Uganda.

Awamu ya 6: Uasi wa wahutu (1990-1994): Tarehe 1 Oktoba 1990, jenerali Fred Rwigyema aliongoza uvamizi wa chama cha RPF cha wakimbizi waliokuwa wakimbizi chini Rwanda. Aliuwawa na kurithiwa na kanali Alexis Kanyarwenge kama mwenyekiti wa chama cha mstari wa mbele cha kizalendo cha Rwanda RPF na tawi lake la jeshi la kizalendo la Rwanda (RPA), lakini kwa ufanisi wa jenerali Paul Kagame aliyekuwa amehudumu kama afisa upelelezi kwenye

kurugenzi ya kiintelijensia ya kijeshi ya Uganda (DMI) kama mwenyekiti wa kikosi cha juju cha maamuzi cha RPA.

Tarehe 3 Agosti 1993, serikali ya Rwanda ilitia saini makubaliano ya Amani ya Arusha pamoja na chama cha mstari wa mbele cha kizalendo cha wanyarwanda. Makubaliano ya ugawanyaji wa madaraka yakavunjika tarehe 6 Aprili, amabapo jenerali Paul Kagame aliamuru kutunguliwa kwa ndege iliyokuwa imembeba rais Habyarimana wa Rwanda, rais Ntayamira wa Burundi na kupelekea kuuliwa kwao wote pamoja na msafara wao wote.

Serikali ya mpito iliyodumu kwa muda mfupi ikaundwa na kamati ya viongozi wa kijeshi chini ya rais Theodore Sindikubwabo, kama taifa lililokuwa linatoka kwenye vita nzito ya wenyewe kwa wenyewe, uzandiki, mafachuko na mauaji ya kimbari na taifa lililoshindwa.

Mauaji yaliyoratibiwa na uanzishwaji wa MRND ulianza mara moja katika kile kijulikanacho kwa sasa kama siku 100 za mauaji ya kimbari dhidi ya watusi. Wahutu wengi waliuwawa na jeshi la RPA ya jenerali Kagame na DMI kwa kile tunachoamini ni mauaji ya kimbari, uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu nchini Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Awamu ya 7: Utawala wa jeshi la wahutu (1994-mpaka sasa): Utawaja wa kijeshi wa rais Habyarimana uliondolewa na jeshi la RPF, likijitangaza kama dola moja mnamo tarehe 4 Julai 1994. Mfano, Pasteur Bizimungu, mhutu, alikuwa rais wa jamhuri ya Rwanda, wakati jenerali Paul Kagame akiwa makamu wa rais na waziri wa ulinzi akabaki madarakani nyuma ya kiti cha enzi. Mwaka 2000, jenerali Kagame alimpindua rais Bizimungu, akamuweka kifungoni kisha miaka mitano baadaye “akampatia msamaha” na kumpekeka kwenye uhamisho wa ndani ambako yupo huko mpaka sasa.

Jenerali Kagame ni mtawala aliyekaa madarakani kwa muda mrefu kwenye historia ya nchi ya Rwanda tangu tutoke kwenye ukoloni.

NJIA NA MIENENDO

Wapo wanyarwanda wengi wasiojua chochote kuhusu hii histoia yetu fupi ndani ya miaka 127. Huenda hata wakaiona kama mzigo wa matukio yanayotofautiana kwenye historia yetu, alama za takwimu zisizo na uhusiano. Wageni, kila wanapopata hamu ya kutaka kuijua Rwanda katika

kila awamu au katikati ya awamu hizi, huyachukulia kama matukio yaliyojitenga, kama picha ya haraka kwenye filamu.

Bado kuna uhusiano uliopo katika awamu hizi:

Kwanza, uwekaji wa maamuzi ya madaraka kwenye mikono ya mtu mmoja tena wa kiimla, tena atokaye kwenye kabila moja, akiwa na tabaka dogo lenye hadhi ya juu wakimzunguka ili kuhakikisha utawala wake unaenea vyema kwa watawaliwa.

Pili, matumizi ya jeshi na matumizi ya nguvu yamesalia kama kifaa kinachoshawishi ili kupata na kuyalinda madaraka juu ya wengineo wengi.

Tatu, kila utawala uliopita iliupasa kutengeneza maelezo yenye kujirudia rudia kama jaribio la kueleza sababu za wao kuwa hapo walipo, alama mpya, dhana na matukio ya kihistoria. Uwepo wa matabaka matabu ya jamii za Abahutu, Abatusi, Abatwa hujidhihirish kwenye historia muhimu ya Rwanda, mpaka sasa madaraka yanapatikana kupitia jina la ama u-Hutu au U-Tusi, na bado inakumbatiwa ili kuendelea kutumia idhini ya utawala wa kiimla.

Nne, Rwanda imebakia jamii iliyopo hatua za mwanzo kiviwanda, ikiwa na Wakulima waliotawanyika kwenye eneo zima la vilima vya Rwanda. Wakulima wa Rwanda mara nyingi watambulika kama tabaka la kiutawala lililojikita mjini kama *abaturage* au *rubanda rugufi,* wenye udhaifu usiosikika nje ya mahakama ya mfalme na hekalu lake. Wakati wa kipindi cha mpito kutoka utawala mmoja kwenda ka mwingine, wale wa tabaka la hadhi huwanyonya na kuwanyanyasa wakulima wasio na amani na kuwafanya kuwatumia kama chambo kwenye gurudumu la machafuko huku wengineo wakiwa wahanga. Kutoka 1959 na kuendelea, wakuliwa walio watusi na wahutu wamekuwa wakimbizi, wahanga wa uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu, mauaji ya kimbari, hali inayoshusha hadhi yao kwenye jamii. Watu mashuhuri Rwanda wanapambania madaraka kwa gharama yoyote kwa kukatana shingo, kufanya pata potea, kufa na kupona, mapambano ya mshindi kuchukua kila kitu.

Tano, uwepo wa nguvu kutoka nje chini Rwanda, kwanza uvamizi wa kijeshi unaoonekana kama utawala wa kikoloni (Ujerumani, Ubelgiji) na baadaye kupitia ushawishi mgumu kupitia fedha, “misaada ya kiulinzi”, usaidizi wa mikakati ya kidunia, (Ufaransa, Marekani, Uingereza), mara nyingi huchukua pande pamoja na tabaka dogo lenye hadhi kuwa madarakani. Katika kushuka, kupanda na muendelezo wa upaganiaji wa madaraka na mivutano ya kikabila nchini Rwanda, nguvu kutoka nje vimewanufaisha vibaraka wachache walioko madarakani, hivyo kuzidisha kutokutaka kukubailana na kulazimisha hali ya usalama. Haishangazi ya kuwa nguvu kutoka nje ni ya kwanza kuwakana wale waliopoteza kwenye janga la kugombania madaraka kadiri wanavyo wakubali washindi wa ushindani wa sasa.

Sita, kwa sababu Rwanda ni sehemu muhimu sana ya *kanda ya intarakastrini* ijulikanayo kama Kanda ya Maziwa Makuu (*Ziwa Tanganyika, Kyoga, Viktoria, Kivu na Edward*), historia yake kwa kiasi kikubwa imefungamana na historia ya wenyeji waafrika wa ukanda huu. Ukanda huu ulikaliwa na watu walioongea lugha ya *Ki-bantu* na katika eneo hili iliwahi kustahimili dola ya utawala wa *Bunyoro Kitara. M*abaya na mzuri ya Rwanda yamekuwa na madhara kwa majirani zetu. Bila bandari na kuwepo ujirani mgumu, ambako migogoro inaongezeka kwa sababu za kutoka nje zitokazo Uganda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Tanzania na Rwanda huiathiri Rwanda. Mara nyingi, majirani zetu wameanzisha ukaribu sana na viongozi wachache wenye tabaka la juu wa Rwanda wakiwa na mikakati binafsi ya kikanda kwenye Kanda ya Maziwa Makuu.

Saba, hatima ya wafalme, marais na wachache walioko kwenye nafasi nchini Rwanda husomeka kama janga jongefu linalokuja juu, huanguka na uharibifu wa tawala. Kipindi cha mwanzo baada ya ukoloni kilianza na mauaji ya kimkakati ya watu wengi pale Rucunshu ambako Mfalme Rutalindwa na washirika wake (wote wakiwa watusi) waliuwawa na kusambazwa uhamishoni. Wajerumani walioikamata na kuimiliki Rwanda wakiwa na Mfalme Musinga ili kiweza kuitawala kikamilifu Rwanda kaskazini, baadaye kuwaacha watawala wa kibelgiji kumtema (1931) na kumfukuzia mbali na kufia uhamishoni. Mwanaye na mrithi wa kiti chake, mfalme Mutara Rudahigwa, alikufa ghafla nchini Burundi mnamo tarehe 25 Julai 1959.

Mamlaka za Ubelgiji walioitawala Rwanda na Burundi wakati ule hawakuwahi kuja hadharani na kuweka wazi namna alivyouwawa. Aliyemrithi Mfalme Kigeli Ndahindurwa alizuiliwa kurudi Rwanda na mamlaka za Ubelgiji wakati akiwa safarini nchini Burundi mwaka 1961 na kuishi kule miaka 50 akiranda randa uhamishoni mahali ambako alifia akiwa na umri wa miaka 80 huko Marekani. Jumuiya yote ya watusi waishio uhamishoni waliuwawa ama kutengwa. Gregoire Kayibanda, rais wa kwanza wa Rwanda huru alipinduliwa na jenerali Juvenali Habyarimana, akamuweka chini ya kizuizi cha nyumbani, akanyimwa chakula na kuuwawa huko alikotengwa. Karibia kila mwanzilishi mwenzake wa mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959 aliuwawa. Rais Juvenal Habyarimana mwenyewe alikuja kuuwawa na jenerali Paul Kagame mwaka 1994, wakati huo utawala wake wa MRND ukididimia mara baada ya kuwaua mamia kwa maelfu ya watusi na wahutu, mara baada ya kukutana na ushindani na kushindwa kutoka kwa RPF, MNRN yote ilikimbilia uhamishoni, huko waliwindwa, kuuawa au waliishia kwenye Mahakama ya Uhalifu wa Rwanda ya Kimataifa au Mahakama za Rwanda za Gacaca. Jenerali Kagame ameendelea kuwatafuta manusura wa MNRD mpaka leo. Wengi wao wamekubali kujificha, kukaa kimya na kujisalimisha mbele ya utawala wake kama njia pekee ya kupona. Wachache bado wanaendeleza imani isiyo kweli kuwa kupitia machafuko na wahutu wenye msimamo mkali watarudi madarakani.

HALI YA NCHI MWAKA 2021

Hali ya Jamhuri ya Rwanda kwa kiwango kikubwa sana ni dhaifu. Miaka ishirini na saba tangu uingie madarakani utawala wa kiimla wa RPF ya jenerali Kagame imeipeleka Rwanda kwenye mtanziko mkubwa wa hofu, wengi kukaa kimya kwa kulazimishwa, taifa zima kukata tamaa na kutokuwa na matumaini. Simanzi ya taifa imeongezeka sana na kujilimbikiza kwa sababu ya karne nyingi ziliacha simanzi ambayo imezidi kuwa mbaya zaidi kila mabadiliko ya utawala yajapo. Wanyarwanda wapo katika hali ya kudumu ya magomvi na uasi wa kudumu.

Hali ya watusi

Tofauti na maelezo rasmi ya kuwa hivi sasa Rwanda imeweza kupata upatanisho na umoja, jamii za watusi na wahutu wamekuwa na utengano mkubwa sana kuwahi kutokea baina yao. Kwa kufutilia mbali utambilisho wa kikabila kutoka kwenye mijadala ya umma na binafsi, utawala wa kiimla unaitaka Rwanda pamoja na dunia kwa ujumla kuukubali uongo wa kwamba utambulisho wa kikabila uliokuwepo umeisha. Ili kuendelea kuwepo, utawala umekwenda mbali na kutumia kila njia kuboresha utengano wa zamani na kutengeneza mpya miongoni mwa jamii za watusi na wahutu.

Kwa mujibu wa maelezo rasmi, ushindi wa majeshi ya RPF wa mwaka 1994 ulirejesha maslahi ya wahutu kwa kuwa ilikomesha mauaji ya kimbari. Mikakati ya jenerali Kagame ya kupata madaraka kwa njia iwayo yote, uamuzi wake kumuua rais Habyarimana, kuvunja makubaliano ya amani ya Arusha, kuikamata dola, kudhihirisha kuwa maisha ya watusi hayakuwahi kuwa kipaumbele chake. Kimsingi, kwa takribani miaka 27 ambayo jenerali Kagame ameendelea kuonesha kutokuwepo kwa kuwajali watusi ambao ni manusura wa mauaji ya kimbari, na watusi kwa ujumla wao. Amehadaa udhaifu wao na kuuthibitisha kwa kusimamisha minara ya mifupa ya watu kwa ajili ya taifa na propaganda za kimataifa ambayo mwishowe huizunguka hofu yao. Mashirika ya manusura wa mauaji ya kimbari yamekamatwa na dola ili vyombo vya kunyamazisha dukuduku au ukosolewaji wa utawala wake kama ukataaji wa mauaji ya kimbari na kudai mabadiliko. Ametengeneza utengano baina ya familia za watusi ambao haujawahi kutokea hapo kabla, kuwashusha karibia maafisa wa juu wa kisiasa na kijeshi waliokuwa sehemu muhimu kwake wakati akitafuta na kushika mdaraka. Njia zake maalumu za kuwaweza watusi ni kuwajengea hofu kwakupitia mauaji ya walengwa, uhamisho, ukosefu wa ajira, kutwaa kwa nguvu au kuharibu mali, vifungo na kupotezwa. Watusi wanaompinga wanashitakiwa kwa rushwa, tamaa, kuyakana mauaji ya kimbari, kupenda mageuzi, ugaidi na kuwakubali wahutu.

Deo Mushayidi, Yvonne Idamange, Frank Rugasara, Tom Byabagamba, Diane Rwigara, Adeline Rwigara, Assinapol Rwigara (wameuawa), Tribet Rujugiro, Alphonse Furuma, Michael Mupende,

Frank Tega, Kayumba Nyamwasa, Gerald Gahima, Patrick Karegeya (wameuawa), Ngabo Rugigana, David Himbara, Theogene Rudasingwa, Josephn Sebarenzi, Dr. Emmanuel Gasakure (wameuawa), Assiel Kabera (aliuliwa), Kizito Mihigo (aliuliwa), Jonathan Musonera na mamia ya watusi walioko kwenye RPF, RPA, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kimsingi imekuwa mhanga mkuu wa vikosi vya usalama vya jenerali Kagame.

Utawala wa jenerali Kagame unajitangaza kuwa ni mkombozi na mtetezi wa watusi wote popote pale walipo na kokote kule walipo ulimwengu, hasa katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Vita ya utawala huu wa kikatili na unyang'anyi ndani wa Kanda ya Maziwa Makuu umeamsha hisia hasi ambazo zitabakia vizazi na vizazi, vikienda mbali na kuhatarisha maisha ya Watusi katika jamii hii mchanganyiko ya ukanda huu.

Hali ya wahutu

Katika kipindi chake cha uongozi, jenerali Kagame kwa siri na hadharani hutaka kuonekana kama ufalme utekao na kutawala ambao umewatawala wahutu vyema na kuwadidimiza na kuwa na hadhi ya daraja la pili lenye majuto.

Utawala huu umewapelekea wahutu walio wengi kuwa kwenye ukimya wa kukandamizwa na kudharaulika. Kwenye maelezo rasmi na hasa kwenye lugha la kificho ya RPF, wahutu wote ni *interahamwe, wauaji wa mauaji wa kimbari, wasiokubali kuwa wauaji* na *wapenda mapinduzi.* Mhutu anayeyakubali maelezo haya hujumuishwa kwa uangalifu kwenye baadhi ya nafasi serikalini ya kuwasaliti wahutu wenzao, na kuwapa uwakilishi kwenye baadhi ya nafasi za chama ili kumchagua jenerali Kagame wakati wa uchaguzi wa chama wa mihula kama utamaduni wa chama kimoja, mgombea mmoja, kutumikia nafasi ya ukibaraka kwenye jeshi lililoko chini ya maafisa watusi na kuwabakiza wakulima katika nafasi yao ya kuendelea kuwa wazalishaji wa chakula na kutoa jasho lao ili kuridhisha matakwa ya watawala.

Wahutu wanaogomea muenendo wa hali hii inawabidi kuvumulia maumivu ya hofu, kukaa uamishoni, kifo, mateso, kufungwa, kupotea na kuchunga vinywa vyao.

Mwenyekiti wa RPF kanali Alixis Kanyarwenge alinyanyaswa, akatenga na mwishowe akafa akiwa mwanadamu aliyejikatia tamaa. Rais Bizimungu alinyanyasika, aliondolewa madarakani na "kusamehewa" na kwenda daima kwenye kifungo cha nyumbani. Kizazi chote cha viongozi wa kihutu waliozikataa falsafa na matendo ya udikteta wa rais Habyarimana na kujiunga na serikali ya RPF mwaka 1994, iligeuka kuwa uchunguzi mfupi na usiyofaa pale walipohoji rekodi ya utawala kwenye haki za binadamu na utawala bora. Kapteni Donat Muvunanyambo aliuliwa mwanzoni kwenye vita ya RPF. Kanali Stanslaus alifungwa gerezani na baadaye kutelekezwa kwenye kifungo cha ndani kama wengineo wengi. Faustin Twagiramungu, Seth Sendashonga, Charles Ntakirutinka, Mark Rugenera na wengine wengi haraka sana waliitwa maadui

(*ibipingamizi, Interahamwe, wauaji, wapenda mapinduzi, wahutu wenye misimami mikali*) hawakuwa na nafasi kwenye uringo wa siasa za RPF. Wengi wao waliondoka nchini na baadaye kujikuta wakiwindwa na kuuliwa kama Seth Sendashonga, Theoneste Lizinde na wengineo wengi.

Watu waliobakia nchini imewabidi kuendana na maisha waliyochaguliwa wahutu, maisha ya kunyamaza na kunynyaswa kana kwamba wanatumikia mifumo ya serikali ya kiimla. Wengineo ambao walithubutu kupaza sauti kama vile Victorie Ingabire, Bernard Ntaganda, Paul Rusesabagina, Dr. Theoneste Niyitegeka na wengine wengi wameishia jela, kudhalilishwa kwenye sare za rangi ya pinki mbele ya mahakama batili zinazouhujumu mfumo wa utoaji haki nchini. Ujumbe wa jenerali Kagame kwa wahutu wote ni rahisi na wa kueleweka: Nimewatawala, nyinyi nyote ni wahalifu, kubalini utawala wangu au muangamie.

Hali ya watwa

Watwa nchini Rwanda ni kundi dogo sana ambalo kwa sasa lipo katika hatua ya mwisho kabisa ya kutoweka. Afadhali hata wafalme wa kitusi wa zamani waliwapa nafasi kwenye maelezo yao rasmi kuhusiana na nafasi na hadhi ya watwa. Wachekeshaji ambao wangemchekesha mfalme na baraza lake, na wakati mwingine waliwaambia watawal pasipo hata kupewa adhabu ambayo wataliwa wengine wangekutana nayo.

Tangu mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959 mpaka utawala wa RPF, taifa la Rwanda na jamii ya Rwanda wamewapuuzia mno watwa, hatua kwa hatua wakajukita wakijikita msituni kwenye sokwe wa milimani na siyo makundi ya kikabila. Serikali ya Rwanda imewaelezea kama watu walioachwa nyuma kwenye historia, hivyo kuwanyima haki yao ya msingi ya kulindwa kama jamii ndogo. Kwa hali tete wanayoipitia ya kupuuziwa na kubaguliwa, utawala unawadidimiza kuelekea kwenye kutoweka.

Uchumi wa kisiasa wa RPF

Mbinu za kupika takwimu zenye kuunga mkono maelezo batili, tabia ya tawala zote za kiimla, imeifikia hatua ya kutisha nchini Uganda. Bila aibu, utawala wa jenerali Kagame umetumia majuto ya mauaji ya kimbari, utofauti wa maisha ya wanyarwanda wa hali ya kawaida, maslahi ya kidunia ya mataifa yenye nguvu kiuchumi, tamaa, kuunga mkono muundo wa maendeleo ambao aidha siyo shirikishi au endelevu. Nyanja zote za washauri wa kimataifa, wataalamu wa Umoja wa Mataifa, maafisa kutoka magharibi, wachambuzi wa masuala ya kijeshi na kiintelijensia, wafadhili, misaada, makampuni ya kimataifa, waangilikana wa Marekani, aina ya

watu wa Hollywood na wasaka matajiri wameufanya mji mkuu wa Rwanda, Kigali kuwa Maka ya Afrika.

Nje ya himaya ya hoteli zenye hadhi ya nyota tano na migahawa yenye nuonekano wa kigeni, wanajichanganya na kufanya mazungumzo na watu wa Kigali waliokaririshwa yale wayaongeayo na ambao wengi wao ni sehemu ya vikosi vya siri vya Rwanda. Wanapoongea sana na kupaza sauti juu ya madai kuwa umaskini nchini Rwanda unapungua, maendeleo ya kiuchumi yanapaa, hali ya kibiashara ni ya kuvutia na kuwa Rwanda inaelekea kwenye hadhi ya nchi tajiri kama Singapore kwenye miaka 30 ijayo. Taasisi za ukopeshaji za kimataifa, mfano Benki ya Dunia, IMF, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na mfumo mzima wa Umoja wa Mataifa imeangukia mtegoni, ukaunga mkono huu mtazamo kimaendeleo. Wanaunga mkono mahusiano ya umma ya Rwanda ili kutoa msukumo kwa soko la Rwanda kama Singapore ya Afrika. Wanawekeza kwenye biashara, uwekezaji wa miradi ambayo aidha si ya kitaifa, kimkakati au yenye kuleta mageuzi. Hakika hii ni miradi yenye kuvutia na kushawishi kumbe inatengeneza hasara si njia sahihi ambayo itaifanya Rwanda kufikia uchumi wa kati ifikapo 2035 au nchi tajiri ifikapo 2050. Hii ni miradi isiyoweza kuleta tija na hivyo kufanana na tembo mweupe ambayo imejengwa kwa ajili ya maslahi binafsi ya jenerali Kagame na kustahimili kwa kundi lake la wachache ndani ya wachache, mfumo wenye kufanana na ule wa kikaburu. Hili ni puto litakalopasuka hivi karibuni na matokeo yake kuwa ya kutisha. Dhana na maelezo ya utawala wa Kagame na wanaomuunga mkono, wote wa ndani na nje, kwa makusudi kabisa huwaonesha wageni yale watakayo kuyaona.

Ipo Rwanda na historia nyingineyo kuhusu hiyo nchi na watu wake. Rwanda inabakia nchi ambayo haijaingia rasmi kwenye mapinduzi ya viwanda ya kulima wa mashambani waishio kwenye uchumi kilimo wa kujikimu tu. Hawa wakulima wengi wao wapo kwenye ardhi ya ekari 2.4 au chini yake, tena kwenye eneo ambalo mazingira ni magumu. Takribani asilimia 82% ya wakaazi wa Rwanda ya milioni 12.5 ni vijijini. Juu ya vilima na mabonde ya Rwanda kuna wakaaji 525 kwa kila km^2 (watu 1,360 kwa kila $m^{2)}$, na kuifanya kuwa moja wapo ya nchi yenye idadi kubwa ya watu. Wastani wa uwezo wa kupata mototo ni juu ya vizazi 4 kwa kila mwanamke kwa mujibu wa takwimu rasmi. Wastani wa umri na idadi ya watu chini ya miaka 25 ndiyo wengi. Idadi ya watu wa Rwanda inakadiriwa kufikia milioni 16 ifikapo 2030, kufikia milioni 23 ifikapo mwaka 2050 na milioni 33 mwaka 2100. Wengi wao katika makadirio haya ya idadi ya watu ni wahutu. Hili ni tishio kwa utawala kwa kuwa ni kibaraka mtusi ndani ya watusi wachache.

Rwanda ni nchi ambapo wanchi maskini huishi chini ya dola mbili kwa siku, ambapo mali za maskini huyo huaribiwa ili kuacha nafasi kwa ajili ya miradi ya jenerali Kagame ambayo ni yenye kuvutia na kushawishi lakini bila tija na mahali ambapo watu wake bado wanasumbuliwa na

funza, chawa na minyoo. Sehemu ndogo sana ya wanyarwanda ndiyo wenye maji tiririka, vyoo vya ndani au umeme. Kutembea peku, njaa, kiu ya maji, watoto wanaopata mlo mmoja kwa siku kama ni bahati yao. Ukosefu wa ajira unapanda kwa kasi, wakati huo walimu, wafanyakazi, wanajeshi, polisi na watumishi wa umma wengineo wakiishi kwa vipato haba.

Kwa hofu na ghadhabu iliyojificha, wanyarwanda huutazama utajiri wa kutisha alionao jenerali Kagame, familia yake, marafiki na vibaraka wanaohakikisha anabakia mdarakani.

Dhana ya nguvu ya nchi kijeshi na jamii yenye nguvu kijeshi

Tangu kuanzishwa kwa Uganda iliyofuatiwa na uvamizi wa Rwanda mwaka 1990, jeshi la kizalendo la wanyarwanda (RPF) limepoteza kabisa dira na misingi yake ya awali. RPA (sasa chini ya jina la vikosi vya ulinzi vya Rwanda-RDF), ilikuwa la kimapinduzi mwanzoni mwa uanzilishi wake kama njia ya mwisho kabisa ya kuishinda ajenda ya kisiasa ya RPF-INKOTANYI ya kuwaunganisha na kuwapatanisha wanyarwanda; kulinda usalama na mali za wananchi, kuleta demokrasia na utawala wa sheria; uchumi wenye usawa na endelevu, kuondoa rushwa, kuwezesha maisha bora kwa wote, kumaliza mwanzo na mwisho tatizo la wakimbizi, kujenga amani, uslama na maendeleo kwenye kanda na dunia kwa ujumla. Alipouwawa jenerali Rwigyema mwanzoni mwa uvamizi wa 1990, na baadaye Peter Bayingana, meja Chris Bunyenyezi na maofisa wa kijeshi wengineo, RPF ilikuwa taratibu inatekwa na jenerali Kagame pamoja na polisi wake was siri (DMI). Jenerali Kagame hajawahi kuja kuwajibika hadharani juu ya mauaji, kukoleza madai ya kwamba yalikuwa na mkono wake. Akiwa na mikono thabiti mbele kwenye mapambano ya kisiasa na kijeshi ikiisha, chama pamoja na tawi la jeshi likapoteza nguvu ya mapinduzi. Hivi sasa chama ni chombo cha kijeshi ambacho taratibu kikawa jeshi binafsi likiongozwa na polisi wa siri ambao majukumu yao ni kujenga na kuimarisha hulka na nguvu ya kiongozi wa juu. Kutoka Kagitumba tarehe 1 Oktoba 1990, mpaka kwenye kukamata madaraka Rwanda na mauaji ya kimbali ya 1994, jeshi la jenerali Kagame halijawahi kuacha kutimiza matakwa yake. RPA imejibatiza kuwa RDP lakini ikabakia kuwa chombo cha kuwahujumu usalama wanyarwanda, kuongeza utawala wa kidikteta, kuendeleza sera za utawala za kijamii na kiuchumi, kumtumikia kiongozi mla rushwa mkubwa kuwahi kutokea kwenye historia ya Rwanda, kutengeneza wimbi lingine la wakimbizi (wahutu), kuipora Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kutenda uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu, mauaji ya kimbari. RPA imepigana Pamoja na majeshi ya Uganda, Zimbabwe, Angola na Namibia. Kwa sasa limekuwa jeshi mamluki likitumikia maslahi ya kifedha ya mtawala mkuu chini ya mwavuli wa kulinda amani ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudani ya Kusini, Mali, Suani na sehemu nyinginezo. Tunapondika sasa, jenerali Kagame anahusika katika njama za kutuma vikosi vya

kijeshi ambavyo vimeajiriwa kama jeshi mamluki kwenda katika jimbo lenye mgogoro la Cabo Belgado kule Msumbiji. RPA imepoteza mwelekeo, kama kinacholifadhili cha RPF.

Mwenendo wa hulka ya jenerali Kagame ikiwepo, dola ipo kamili kijeshi huku jamii kwa kujua na kutokujua inaandaliwa kwa ajili ya machafuko na migogoro. Siasa, maendeleo ya kiuchumi, muingiliano wa kijamii na karibia kila Nyanja ya maisha ndani ya Rwanda inafaidisha nguvu hii ya watusi inayomuathiri kila mtu. Polisi wa siri, majeshi, RPF na wawakilishi wa serikali kila mahali hutumika kufanikisha matakwa ya kiongozi mkuu. Utawala unaopiga hatua kwenye hofu na woga huwaaminisha watusi ya kuwa kimsingi wanakabiliwa na tishio kutoka kwa wahutu, na kutoka kwa baadhi ya watusi wanaoupinga utawala wanaitwa wanaojitetea dhidi ya madai ya wahutu.

Imani potofu ya *Ingando* (kambi za mafunzo ya kinguvu na propaganda ya falsafa na imani za kijeshi na kisiasa);

Intore (mawakala wa polisi wa siri wa nyumbani na ugenini); Misingi na mafunzo ya RDF; Polisi wa taifa: Siku ya wanyarwanda waishio ughaibuni, vitengo (LDU); Walinzi maalumu wa rais na vikosi vyake; mitandao ya polisi wa kintelijensia walio rasmi na wasi rasmiwaliosambazwa kila kilima (nyumba kumi) na maeneo yaliyo zaidi ya Rwanda na Kanda ya Maziwa Makuu mpaka sehemu nyinginezo na dunia kwa ujumla; biashara; mashirikia; makundi ya kitamaduni; mashirika ya kimataifa; vyombo vy habari vya umma na binafsi; makanisa; misikiti; wawakilishi wa kidiplomasia wa Rwanda; taasisi hizi zote zinao mtandao wa watusi waliojiandaa kushika, kumaliza nguvu uasi wa wahutu kwa ujumla na watusi wanaopinga itakapolazimika. Wananchi wakitusi walio wengi wamepokea mafunzo ya msingi na kupewa silaha. Wakati ambao idadi ya jeshi hili rasmi na lisilo rasmi haijulikani kwa sababu za asili ya usiri mkubwa wa utawala huu, japo hukadiriwa kujumuisha watu takribani 500,000. Kwa matumizi ya ulinzi, idadi hii inavuka kiasi rasmi, walipa kodi wa Rwanda, deni la nje na misaada ya nje husaidia kuelezea ugumu wa huu mfumo hamasishi wa kijeshi.

Pamoja na kuipa jamii utayari wa kijeshi, hali hii ya kulijenga taifa kijeshi imepenya ndani ya Rwanda kwa sasa. Neon *Afande* (….) na DMI ndiyo hutumika sana, kuheshimika, kuogopwa kwenye jamii ya Rwanda. Jenerali Kagame ni dhahiri ndiye *Mwami* (mfalme), *kiongozi wa juu kabisa, Afande, kamanda mkuu wa DMI, Amiri Jeshi Mkuu, Mwendesha Mashtaka Mkuu, Jaji Mkuu, Mkuu wa Magereza* yote kama mtu mmoja. Anayo haki ya uatawala pekee kwenye Nyanja ya machafuko na huaminika kwamba alitawalaye jeshi hujimilikisha nguvu yote ya Rwanda, na hujiona yeye asiye na mipaka. Watusi walio maafisa wa jeshi wanaoendesha ghasia wanajua fika ya kuwa ni lazima wawe sawa na matakwa ya mtawala mkuu. Upande binafsi, jenerali Kagame na maofisa watusi maranyingi huigusa historia ya Rwanda ambapo hudai ya

kuwa uthabiti wa jeshi la watusi uliwafanya wahutu watawale kuanzia mapinduzi ya 1959 mpaka kwenye anguko la utawala wa jenerali Habyarimana kuwa wa muhimu na siyo utawala.

Rwanda hujenga picha ya kuwa inaendeshwa na taasisi ambazo zimekamilika, kila upande ukimkagua mwenzake baina ya mihimili ya Serikali, Bunge na Mahakama. Ipo katiba na sheria ambazo ziliandikwa ili kumpa nafasi jenerali Kagame kuwa mtawala wa juu anayeajiri wajumbe wa bunge, seneti, majaji, mawaziri. Kila mtu aliyeko Rwanda, wa hali ya juu ama chini anatambua ya kwamba anamtumikia jenerali Kagame na anaweza kufukuzwa wakati wowote pasipo kupewa notisi.

DMI: Polisi wa siri wa rais Kagame

Kama ilivyotajwa hapo awali, utawal wa kiimla wa jenerali Kagame unasalimika kupitia mfumo wa kuwajengea hofu ambayo hujijenga kupitia machafuko yaletwayo na kikosi cha siri cha polisi: Kurugenzi ya Intelijensia ya Kijeshi. Mwanzo wake unaanzia kule Uganda ambako RPF na tawi la jeshi lake la RPA yalizaliwa, DMI inayoogopwa sana imepitia mabadiliko ya majina mbalimbali, lakini kila mnyarwanda anajua intelijensia ya utawala huu katika muundo rasmi na usio rasmi na katika jina lake. Jenerali Kagame ameajiri na kufukuza viongozi wake lakini malengo yake yamesalia kuwa msingi thabiti ambao mtawala mkuu ameutumia kuitawala RPF Rwanda kwa ujumla wake kwa miaka 31.

Alisyeendelea kuwepo kwenye DMI ni jenerali Kagame. Pamoja na wakurugenzi waanzilishi wa intelijensia ya kijeshi, jenerali Kayumba Nyamwasa, wote wawili wamepelekea muelekeo wa kesho ya shirika hili kuwepo kwa miongo mitatu. Kupitia DMI wameweza kusalia kwenye mlengo wa maono yake yasiyoyumba ya kusimamia maelezo rasmi, kuhodhi nyanja zote za matumizi ya nguvu, vurugu, kuhodhi njia zote za habari na mawasiliano, kuibadili Rwanda kuwa taifa la chama kimoja, kuweza kudhibiti uchumi kikamilifu, uporaji wa maliasili kule Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kufanya uhalifu dhidi ya wahutu pasipo kuwajibika, kuwatia hofu au kutishia jamii ya kimataifa, kuwatesa na kuwaua kikatili washindani wake, kutandaza hofu na woga miongoni mwa jamii ya watusi, kuua asasi za kiraia, kupenya na kuingilia mashirika ya dini, kupenya na kuingia kwenye mashirika ya kimataifa na kuwaondoa kazini viongozi waandamizi wa kihistoria wa kisiasa na kijeshi wa RPF na RPA.

Kuuhujumu Ukanda

Kama polisi wa siri wa jenerali Kagame, DMI ina macho, masikio, mikono na miguu katika ufalme mdogo anaoutawala. Shirika hili liliratibu mauaji ya Juvenal Habyarimana wa Rwanda na rais Cyprian Ntaryamira wa Burundi (1994), rais Laurent Kabila wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (2001). Tangu mwaka 1996, polisi wa siri wa Rwanda pamoja na jeshi wamekuwa katika sehemu muhimu ya vita kuu mbili vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, tangia hapo

wameendeleza harakati za uwakilishi wa kijeshi. Idadi ya vifo baina ya watu wa Kongo inakadiriwa kufikia million 5 mpaka milioni 6. Ukatili, vitisho na misimamo ya utawala wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Angola, Zimbabwe, Namibia, Burundi, Uganda, Tanzania, Afrika ya Kusini inadhihirisha sera yenye lengo la kuuhujumu ukanda wa Maziwa Makuu na hasa Afrika kwa ujumla. Fikra za jenerali Kagame na kujifanya kuwa yeye ni mwana umajumui wa Afrika ni mazigazi.

Mifumo ya kidunia

Misheni za nje za Rwanda, misheni za kigeni na mataifa mengine nchini Rwanda, biashara, wanyarwanda waishio ughaibuni, taaluma, taasisi za mahusiano ya umma, washawishi na washauri wa mambo na njia nyinginezo ni maeneo muhimu sana kwa ajili ya mapandikizi yawezayo kusaidia polisi wa siri wa jenerali Kagame. Mfano wa watu ambao wamekuwa muhimu sana kwa kuuza mema ya jenerali Kagame na kupaza sauti propaganda za polisi wa siri wa utawala ni rais mstaafu wa Marekani Bill Clinton, waziri mkuu staafu wa Uingereza Tony Blair, rais wa zamani wa Ufaransa Nicolas Sarkozy, rais wa sasa wa Ufaransa Emmanuel Macron, Rick Warren, Susan Rice, Clare Short, Andrew Mitchel, Howard Buffet na wengine wengi kutoka nje wajulikanao kama Baraza la Ushauri la Rais (PAC).

Kupitia mitandao ya kimataifa, polisi wa siri wa jenerali Kagame huwezesha kueneza propaganda, kukabili upinzani wa aina yoyote, kukusanya rasilimali za kutumiwa na vyombo vya serikali ya kiimla, kuwaua wanao dhaniwa au kuwa maadui wake waliopo uamishoni pamoja na kulimbikiza utajiri kwa ajili ya mtawala mkuu na familia yake.

Upinzani wa Rwanda

Tangu mapinduzi ya Rucunshu ya mwaka 1896, Rwanda imezalisha mawimbi ya wakimbizi. Wakati wa utawala ya kikoloni Rwanda walisafirisha nje wakimbizi kwenda nchi za jirani katika ukanda wa Maziwa Makuu ili kutafuta maisha yenye unafuu. Kulazimika kuhama kwa hali ya juu cha watu wa Rwanda na kuwa wakimbizi au kuhama kwa ndani kwa ndani ni hali iliyokuwepo mara baada ya mapinduzi ya wahutu ambayo imedumu mpaka leo.

Siasa za misuguano na kikatili za Rwanda zimezalisha washindi na washindwa wa kudumu. Washindi huchukua kila kitu na wanaoshindwa hufukuzwa na kupewa hadhi ya ukimbizi au uhamisho wa ndani ya kifungo au kukaa kimya. Maujai ya kimbari, uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya utu, jela, kupotea, kunyang'anywa mali, unyanyasaji na kila aina ya uvunjaji wa haki za binadamu huwafuata wale wanaoshindwa katika minyukano hii ya ndani kwa ndani ya kisiasa. Kwakuwa kila awamu ya utawala huingia madarakani kwa visingizio vya kutaka kushughulikia malalamiko ya wahutu na watusi, kufanikiwa kwake ni harasa kwa upande mwingine.

Hili lina madhara matatu. Kwanza, kuminywa kwa mwanya wa kisiasa unazitoa mhanga sauti za upinzani ndani ya nchi. Na kila utawala umefanya kujitoa mhanga kuongezeka sana. Nafasi pekee iliyopo ya kueleza yaliyo tofauti kwa maofisa ni kuwa nje ya Rwanda.

Pili, kwa kuwa kupata au kukosa madaraka ya nchi kuna sura ya wahutu au watusi, sauti za kudai haki za ughabuni huwa inawakilisha manunguniko ya wale waliokosa madaraka. Kwa kadiri muda unavyoenda, hii huzidisha misimamo kwa watu ambao ni lazima waongee simulizi zenye mateso, kukandamizwa na kupokwa udugu na ujamaa wa jamii yao. Muonekano wa siasa za Rwanda za ughaibuni ni wa makundi yenye kujitambua na kuja pamoja kupambania matakwa yao badala ya yale ya kitaifa ambao ni uchaguzi wa msingi na ujulikanao sana.

Tatu, kama ilivyodaiwa hapo awali, mpaka sasa madaraka nchini Rwanda yamekuwa yakipatikana kwa njia ya mapinduzi ya kikatili na nguvu za kijeshi. Hii imebakia kuwa mantiki ya msingi ya mabadiliko ya utawala. Kama upekee kidogo, lile linaloitwa tabaka la upinzania la Rwanda bado limenaswa katika mantiki ile ile iliyokuwa imedhihirishwa pale Rucunshu na wakoloni wa Ujerumani na Ubelgiji, mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959, utwaaji kwa mdaraka wa jeshi la wahutu wa kaskazini na ushindi wa jeshi la watusi mwaka 1994.

Mwaka 1994, kushindwa kwa utawala wa wahutu wa MRND ulihitimisha ukurasa wa utawala wa wahutu ambao ulianza na mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959. Imekuwa miaka 27 sasa tangu jeshi la watusi la jenerali Kagame lilishinde jeshi la wahutu la jenerali Habyarimana. Hakuna majeshi katika historia nzima ya Rwanda yamewahi kuwasababishia mateso ya kibinadamu kama majeshi haya mawili. Kwa ushindi huo, jenerali Kagame hajapata somo kutoka kwa mapito ya Rwanda, kwamba wafalme wa watusi waliotawala kwa karne nyingi mwishowe walipoteza dhidi ya ukuu wa majeshi ya nje, na mwishowe kuibuka kwa tabaka la wahutu ambalo liliweza kuhamasisha sehemu kubwa ya jamii ya wahutu walionyanyasika.

Kukatwa vichwa, kushindwa na kutawanywa kwa jeshi la wahutu la jenerali Habyarimana haukuwepo tena. Sehemu ya wachache walionusurika kwa wingi wapo mafichoni na ukimya bado hawajapata somo la kuwa kwa ufinyu mkubwa madaraka hupatikana kama kuwa vibaraka, kujifanya kuwakilisha kundi la kikabila na hata wengi wao kama njia ya kushinda.

Kukamata kwa madaraka ya taifa kupitia machafuko kunaishi katika upinzani wa Rwanda. Kwa kuendelea kushika mdaraka kupitia machafuko ni sababu ya kuwepo kwa utawala wa jenerali Kagame. Kwenye eneo la machafuko, jenerali Kagame ndiye mwenye mkono wa juu kwa sasa. Na muhimu sana huwezi kutibu na kuponya simanzi ya Rwanda iliyotekelezwa na machafuko kwa kufanya machafuko mengine.

Wasifu wa jenerali Kagame.

Generali Kagame ni mtu aliyetokea kwenye umaskini ambaye amekuwa mkimbizi alipokuwa kijana mdogo, akakulia kwenye kambi ya wakimbizi na kusomea Uganda. Kama wengineo wa kizazi chake, wazazi wake walikuwa watusi walikimbia Rwanda mara baada ya mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959.

Tabia yake ilijengwa kwenye kambi za wakimbizi, katika maisha yake na mahangaiko ya uhamishoni, vichaka vya pembetatu ya Luwero kule Uganda ambapo jeshi la upinzani la kitaifa la Yoweri Museveni lilipigana vita ya porini yenye mafanikio na kutwaa madaraka mwaka 1986, uvamizi wa RPF ya Rwanda ya 1990, na kifo cha ghafla cha kiongozi wao madhubuti jenerali Fred Rwigyema. Jenerali Kagame ni kiongozi wa bahati aliyebadili muelekeo wa harakati za kimapinduzi aliyejikuta kwenye mabaya kutokuwepo kwa uongozi katika kipindi muhimu sana cha ujenzi.

Wafuasi wake mashuhuri wamemfananisha yeye na kiongozi wa kikabila Kigeli Rwabugiri, mfalme mashuhuri wa watusi kwenye historia ya Rwanda katika nusu ya pili ya karne ya 19. Mwaka 1929, mmoja wa wanahistoria wa Ulaya J.M Derscheid alimuelezea mfalme kwa maneno haya;

> "Ili kuimarisha nguvu ya kijeshi ya nchi; kuziweka taasisi kuu za ufalme juu ya usaidizi wa vipengele vya kilimo hivyo kuwafanya kuwa sehemu ya hadhi ya chini; taratibu kupunguza nguvu ya koo za ukabaila na wafalme wa majimbo huko nyumbani na wakati huo huo kuhamisha nguvu ya watusi kutoka kwenye mambo ya ndani na kuwapeleka nje kwa ajili ya malengo ya kivita…." (Ren'e Lemarchard, *Rwanda na Burundi,* uk.20)

Wakili wa kwanza wa kikatoliki nchini Rwanda, Leon Classe, alimchambua Mfalme Rwabugiri katika maelezo yake:

> "Rwabugiri alikuwa mtawala wa kifamle, mwenye kuwatakia mema watu, mbabe kwa watusi. Watu hawa walimpenda kwa sababu yeyote aliweza kumkaribia na kutamka malalamishi yake na manunguniko aliyonayo mbele yake. Watusi walimuogopa kwa kuwa matamshi yake hayakuthamini maisha ya mwanadamu…. Hakusitisha kuwa vitani na majirani zake, Rwabugiri aliwaongoza wanyarwanda kila mahali na fursa za kipekee ili kujikusanyia mali wakati wa mapigano…." (……)

Kwingineko kwenye historia ya ulimwengu mtu anaweza kupata maelezo ambayo hukaribia kuuelezea mtazamo wa jenerali Kagame na sera zake. Peter mkuu wa Urusi (1672-1752) illielezea dira ya Urusi hivi:

> "Taifa la Urusi inabidi liendelezwe katika hali ya vita ya kitaifa ili kuwapima uwezo na uimara wa wanajeshi; vipindi vya mihula hutumika kuimarisha uchuni wa taifa, kulijenga jeshi, kuchagua

eneo sahihi la kuvamia. Hivyobasi, amani ipo kusaidia vita na vile vilevile vita kusaidia amani, yote ni kwa maslahi ya kupanua ukubwa na kustawi kwa Urusi." (Daniel Chirot, *Ubabe wa Kisasa*, uk.50)

Mshauri wa watawala wa himaya ya Qin, China, mungu wa Shang, kwenye karne ya nne Kabla ya Kristo aliandika:

"Nchi inapojengwa kikamilifu ni pale kupitia kilimo na vita…. namna ya kuiongoza nchi ni kutokuwa na leseni ya kusema. Hii ni kwa ajili ya watu wasiwe na mambo mengi na wasipoteze lengo. Njia ya kuongoza nchi vyema ni kwa sheria za maafisa kueleweka; hivyo asiwepo wa kutegemea uelewa wake na mawazo ya watu wanaofikiri. Mtawala huwafanya watu wawe na akili moja na hivyo wasije kufanya mambo kwa maslahi binafsi. Hivyo uwezo wa nchi utaimarika." (Daniel Chirot, *Ubabe wa kisasa,* P.5)

Dikteta wa kifashisti Benito Mussolini amejulikana mara nyingi kwa kusema kuwa *"kila kitu ndani ya nchi, nje ya nchi kisiwepo chochote na kisiwepo chochote dhidi ya serikali"*

Akitenganishwa na muda na nafasi, Rwabugiri, mkuu Peter, mungu wa Shang, Mussolini na jenerali Kagame wana sifa sawa zenye kufikirisha. Hawatakii mema kwa mtu yeyote na wakatili kwa hata waonekanao kidogo kupinga. Kagame anatawala kwenye karne ya 21 akiwa na vyombo vya kudhibiti na kufanya vita kwa kiasi ambacho wote waliomtangulia wasingeweza kufikiria. Ni mtu mwenye hasira, katili, mwenye manyanyaso ya kimwili kwa majenerali wake, mwenye visasi, mwenye wivu, asiyejiamini na alifanikiwa kutawala kikatili. Kwa kadri alivyokaa madarakani ndivyo amejikusanyia hamu ya kutumia mabavu kupata utajiri kwa ajili yake binafsi na familia. Kwake yeye, taifa la Rwanda ni yeye. Afande ni taifa.

Miongo yake mitatu ya utawala wa hofu umeacha damu na machozi kwenye njia yake; simulizi zenye uongo na kupotosha ambazo huwafanya wahutu kuwa wahalifu pamoja na wapinzani wake kiujumla; kwa kutokuchoka kwa polisi wake wa siri (DMI) katika kutekeleza ukatili na kuanzisha vita kitaifa na kikanda; *"Madai ya kufikirika na kupakazia ya watusi"* ya uongozi wa kijeshi huku ukiondoa washindani wa kweli na wenye uwezo; kuibadili RPF inayotawala kuwa muhuri mpira wa polisi wa siri ambao husimamia matakwa yake huku wakiwaondoa washindani wa madaraka walio wa kweli na wale wawadhaniao ; kuchukua kwa nguvu na kuleta pamoja bunge, serikali kuu na mahakama chini ya mtu mmoja; kuifanya nafasi ya kisiasa kuwa finyu, asasi za kiraia, vyombo huru vya habari, ufikiri, udhibiti binafsi wa himaya ya kifedha ambayo imesambaa nchini kote na kwenye sekta binafsi pamoja na mtazamo wa auaye mfululizo, muuaji wa watu wengi ambaye pasipokuchoka hutenda pasipo kuwajibishwa.

NJIA YA KWENDA MBELE: KUIFIKIRIA RWANDA MPYA

Kwa sasa Rwanda haijawa katika ubora wake stahiki. Katika mageuzi ya ulimwengu na historia ya mwanadamu, ni maendeleo ya kijamii ambayo yametokea kwa karibu katika bara la Afrika. Sisi ni Waafrika, tuishio katika ukanda wa maziwa makuu.

Ndiyo maana historia ya Rwanda ina uhusiano mkubwa na majirani zetu na kesho yetu ina uwiano wa kimuunganiko na watu wa ukanda huu. Siyo tu kwamba historia ya Rwanda inahusu simulizi za wafalme wa Kitusi, watawala wa kikoloni, mageuzi ya kikatili, watu mashuhuri walioiongoza Rwanda mara baada ya utawala wa kikoloni. Ni mkusanyiko wa simulizi za Wanyarwanda katika muingiliano baina yao wenyewe, waafrika wenzao na asili yao.

Sisi ni jamii ya aina gani? Kwa kutazama yaliyopita na kutafakari upeo wa nyakati za sasa, ni dhahiri kuwa wanyarwanda pamoja na wasio wanyarwanda wamejaribu kutumia kila aina ya mbinu kutengeneza muelekeo wa historia yetu. Tumeuliwa na kuuana kwa jina la uzalendo na masilahi ya makundi binafsi, wanyarwanda wameua watoto wao, marafiki, ndugu, majirani. Rwanda imejikwaa kutoka kwenye utawala wa kifalme, kuwa chini ya milki ya kikoloni kwenda kwenye kujitawala wenyewe bila kupitia mwangaza wa amani, uhuru na upendo kama vitu vya msingi sana na visivyokwepeka katika kuijenga Rwanda.

Tunaishi kwenye eneo dogo liitwalo Rwanda na tumeshindwa kubuni fursa zisizo na kikomo ili kujenga jamii endelevu na thabiti. Tunazungumzia uthabiti wa tamaduni na hulka za wenyeji wa Rwanda kabla hazijaharibiwa na ujio wa utawala wa kikoloni, lakini tupo kimya juu ya kutokuwepo kwa usawa ambao umekuwepo katika historia yetu. Tumerithi mitazamo ambayo inatupelekea kuchukuliana wenyewe kwa wenyewe kama “watu baki”, watu wakuja tu na wasio wazawa. Tumeijaribu dini na bado tumeshindwa kuielewa maana kuu ya kanuni isemayo “mpende jirani yako na mpende Mungu wako” ambayo imo katika imani zote za dini. Tumehangaika katika kujieleimisha wenyewe lakini bado tunapata anguko la hisia za ubinafsi na kufumba macho yetu juu ya bahari kubwa ya umaskini, magonjwa na ujinga unaotuzunguka. Kumbukumbu tulizonazo ni ubaguzi kiasi cha kukumbuka ukweli mdogo wa hapa na pale lakini kushindwa kutambua maumivu na majonzi ya wanachi wenzetu.

Tunafurahia matumizi ya bidhaa na huduma ambazo zimetengenezwa na jamii zilizopiga hatua pasipo kijikita kwenye kuwekeza katika uhuru uliopo kwenye ugunduzi wa mikakati inayoleta msukumo kwenye jamii husika kwenye nguvu ya kiuchumi. Tunaongea lugha moja lakini bado tunashindwa kuvuka kikwazo cha kutokuaminiana ambacho tumekitengeneza katika kuongea na kusikilizana. Tunatambua mfumo wa kimamlaka ambao umerundika madhira na maumivu makubwa kwa kizazi kimoja baada ya kingine cha Rwanda na bado tunaendeleza kupuuzia na

kutojali, tukiamini kuwa makundi mengine, wanasiasa, wataalamu wa majeshi au watu kutoka nje watafanya miujiza ili kutukomboa.

Iwapo mfalme Musinga, wakoloni wa Ujerumani, Ubeligiji, mfalme Ludahigwa, mfalme Ndahindurwa, makanisa ya Kikristo, Raisi Gregoire Kayibanda, jenerali Juvenal Habyarimana, jenerali Yoweri Museveni, jenerali Paul Kagame, Ufaransa, Uingereza, Marekani, Afrika, vita ya yenyewe kwa wenyewe, mauaji ya kimbali na dhana jumuishi nyinginezo pamoja na makundi ambayo hawajatoa haki na suluhu ya kudumu kwa wanyarwanda. Nani ataikomboa Rwanda kutoka kwenye muendelezo wa utawala wa kimabavu, ukatili, utovu wa nidhamu uliokithiri na umaskini? Ni nani atawaleta pamoja na kuwaponya watu wetu? Nani atawaletea uhuru wanyarwanda wote na kujenga jamii yenye mshikamano endelevu na amani yao wenyewe na majirani zake? Wanyarwanda pekee ndiyo wanaweza na ni lazima.

Ni lazima tujizatiti kuweka malengo ya ushiriki katika mabadiliko yenye amani na siyo ghasia. Rwanda imekuwa na mapinduzi ya kutosha yenye ghasia. Ni lazima wanyarwanda wakatae fikra ya kwamba utawala pekee ambao unapatikana kwa njia ya ghasia, ukalindwa kwa njia ya ghasia na ukatili ili kuleta mabadiliko ya kiutawala ndiyo njia pekee. Ni lazima wanyarwanda waweke historia yao na ile ya taifa lao kwenye usahihi wake, katika uzuri na ubaya wake. Wanyarwanda hawana budi kuikubali historia yao pasipo kuwa mateka kwayo. Upo ugumu katika kusimulia simulizi zao lakini hakuna njia nyingine mbadala.

Itabidi wanyarwanda watambue ya kwamba mfumo wa kisiasa utumikao kwa sasa ambao vyama vya kisiasa vya ndani na nje hushindana na utawala wa jenerali Paul Kagame uangaliwe upya kwa ubunifu. Harakati za kijamii zenye maelezo ya kimantiki na maono shirikishi kwa wanyarwanda wote itafanikiwa. Muungano binafsi wa kimaslahi, mipango na njama zilizoandaliwa ili kukamata dola kupitia ghasia na hadaa za jamii na kikabila zimeonesha kutozaa matunda, hata pale walipo fanikiwa kukamata dola.

Kwa kuwa tu taifa lenye wakulima maskini, msingi wetu wa kujenga maendeleo ya watu unaanzia hapa. Wastani wa umri nchini Rwanda ni miaka 20 katika idadi ya watu inayokadiriwa kufikia milioni 23 ifikapo mwaka 2050. Mtoto wa Kinyarwanda anayezaliwa siku ya kuchapishwa kwa andiko hili ama ataishi maisha mafupi ya shida au ataishi mpaka miaka 80 kuikumbatia karne mpya mwaka 2100 kulingana na uamuzi tuufanyao leo. Kupanga ni kuchagua. Njia za kawaida zilizozoeleka hazitaweza. Mbinu bunifu na za haraka zinahitajika ili kupiga hatua.

Ni lazima wanyarwanda waache maramoja kukumbatia njia ya kuwa suluhisho la matatizo ya Rwanda ni kumtafuta kiongozi mpya kutoka kwa mfalme, rais, mkombozi au shujaa. Wanyarwanda wanachohitaji ni mwangaza mpya na uzalendo shirikishi, mazingira ya kidemokrasia, utawala wa sheria, uhuru wa vyombo vya habari, asasi za kiraia huru na uongozi

baina yao wenye kujali, kuthamini na hekima katika kutafuta suluhu ya kukabili simanzi, uoga, kutokuaminiana na uongozi wa kimabavu. Rwanda inahitaji uongozi unaoleta pamoja, kuponya taifa na kuisemea simanzi kwa ujumbe wa matumani. Uongozi unaoweza kufikiria jamii mpya ya wananchi huru ambao watashirikiana kuutengeneza upya muungano wa jumuiya ya kisiasa ya Afrika Mashariki.

Wakati tunatazama mbele ya muongo mmoja kwenye miaka ya 2030, 2050 na 2100, hizi ni baadhi ya changamoto zinazoikabili Rwanda, mawazo chanya ya kuzingatia katika mijadala baina ya wanyarwanda, jirani zetu na ulimwengu kwa ujumla wake;

1. *Kukomesha utekaji nyara, vita na mauaji ya kimbari.*

Wanyarwanda wanashikiliwa mateka katika ardhi yao, wapo walioko kwenye uamishoni wa ndani na nje. Uanzishwaji wa chama cha siri cha kijeshi chenye kujiimarisha kila idara ndani ya dola ambacho kinahakikisha watu wote wanakuwa chini ya uangalizi na ufuatiliaji maalumu. Uelewa thabiti wa tatizo la kuchukuliwa mateka ni muhimu, na hili linaanza na uandaaji wa wasifu wa kisaikolojia wa mteka nyara mkuu na washirika wake wa karibu. Jenerali Kagame anayo damu mikononi mwake kiasi kwamba hatoshindwa kumwaga damu nyingine tena. Utawala wake utafika kikomo. Kwa njia gani na lini inategemea na kiwango cha ubunifu wa kifikra na matendo ya wanyarwanda wenye utayari.

- Kuimarisha intelijensia
- Kuanzishwa kwa mifumo ya mawasiliano na wadau wa nje na ndani ya Rwanda
- Ujenzi na uimarishaji wa mifumo shirikishi
- Uenezaji wa diplomasia ndani ya jumuiya ya Afrika ya Mashariki
- Usambazaji wa polisi wa siri, ramani na rasilimali
- Uhamasishaji, uandaaji, uimarishaji na uunganishaji wa mijadala ya amani ili kutengeneza ajenda ya kitaifa ihusuyo hali ya nchi baada ya kipindi cha Kagame
- Uhamasishaji wa rasilimali

2. *Uvunjaji wa kikosi siri cha polisi cha jenerali Kagame na taasisi za kiusalama za mlengo wa kulia*

Jeshi la siri la polisi la Rwanda pamoja na mitandao yake yote lazima iivunjwe mara moja mara baada ya kipindi cha Kagame. Mpaka sasa taasisi za kiusalama za Rwanda zimegawanyika, hivyo kukosa sifa ya utaifa. Hivyobasi, taasisi zote za ulinzi ni lazima ziwe rasmi, zisijihusishe na

uhalifu, zifanye kazi kitaalamu, ziwe na uwakilishi wa kitaifa kama taasisi za kitaifa na ziwe chini ya usimamizi wa bunge lenye uwazi.

- Uvunjaji wa mitandao yote isiyo rasmi
- Uvunjaji wa vikosi vya ulinzi vya mitaani
- Kuweka wazi taarifa zote zilizopo zinazohusiana na shughuli za kiuhalifu zilizoanzishwa na polisi wa siri na kuwafikisha wahusika mbele vyombo vya haki
- Kupunguza ukubwa wa jeshi la vikosi vya ulinzi na kuiweka wizara ya ulinzi chini ya uangalizi wa jamii
- Kuzuia vita na utumikaji wa jeshi la taifa katika shughuli za kijeshi za nje ya mipaka pasipo idhini ya bunge
- Kulizuia kisheria jeshi kushiriki katika harakati za kisiasa na kujihusisha na vyama vya kisiasa.
- Kuzileta taasisi zote za kiintelijensia chini ya usimamizi jumuishi wa mfumo wa kiuongozi wenye uangalizi maalumu wa kibunge
- Kuboresha kitaaluma na kupunguza idadi ya polisi kwa kutumia udhibiti imara wa kibunge
- Kupunguza ukubwa wa bajeti jumuishi wa taasisi za kiulinzi
- Kuwajumuisha kwa makusudi Wahutu katika ngazi ya kati naya juu ya uongozi wa taasisi zote za kiulinzi
- Kutengeneza wizara mpya ya maslahi ya veterani ili kuhusika na idadi kubwa ya wanajeshi watakao sitishiwa kazi kutoka RDF, walioachishwa kutoka iliyokuwa FAR na makundi ya waasi.

3. Kulileta taifa pamoja

Kama taifa, Rwanda imekuwa katika miongo ya kutawanyika na utengano. Siyo tu miongo lakini pia vizazi vimepotea. Ni muda sasa kuanza mchakato wa kuwarudisha wanyarwanda kwenye ardhi yao ya nyumbani. Ni wakimbizi pekee na wale waishio ughaibuni ambao wao wana uhuru wa kurudi nyumbani pale wanapowiwa. Ni nchi yao wote wananchi waishio katika uhamisho wa ndani kama mateka pasipo uhuru wa kufikiri na kufanya yale wayatakayo.

- Kufanya mazungumzo na wakimbizi, nchi wahifadhi na jumuiya ya kimataifa kwa ajili ya kurudi nyumbani kwa kujitakia
- Katika mfumo thabiti wa kikanda, pamoja na usaidizi wa jamii ya kimataifa, kufanya mazungumzo ya amani na majeshi asi ya Rwanda yaliyojikita mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo ili kusitisha misuguano. Kubuni njia za ajili za usitishaji wa shughuli

za kijeshi, ujumuishaji na uingizwaji mpya katika maisha ya kiraia au kujiunga na jeshi jipya la RDF.

- Majadilliano na jamii ya kimataifa kwa ajili ya kuwarudisha nyumbani kwa hiari wale amabo wamehukumiwa au kuachiwa huru na Mahakama ya Uhalifu ya Kimataifa ya Rwanda. Wale wanaotumikia adhabu ya vifungo wanaweza kumalizia vifungo vyao Rwanda, wakati wale walioachiwa huru wanaweza kuanza mchakato wa uponyaji wa masaibu, ujumuishwaji katika maisha mapya na wana fimilia wao.

- Kupitia misheni za kidiplomasia za Rwanda na wawakilishi wao, kuwezesha wanyarwanda wote walioko diaspora kupata pasipoti, kusafiri kwenda Rwanda kwa urahisi, kushiriki katika nyanja zote za maisha ya nchi yao.
- Mashirika yote yaliyoko ughaibuni yenye ushirika wa karibu na vikosi vya siri vya polisi vipewe hadhi ya ujinai.

4. Kusema ukweli kwa ajili ya haki na uponyaji

Tengeneza mazingira salama kwa ajili ya ukweli kusemwa kwa lengo la kufufua badala ya kudumaza. Jinai zote dhidi ya watu lazima zitambuliwe, wahusika waletwe mbele ya vyombo vya haki kupitia mfumo wa haki na uwazi.

Kumbukumbu na kumbukizi ni haki ya kila mnyarwanda. Kwa hiyo ni msamaha. Kwa nchi yetu, kutafuta muafaka ni kujitoa mhanga kwenye njia ya ukusanyaji wa kumbukumbu na kumbukizi. Hakika yaweza kuwa ahueni lakini yaweza kutengeneza njia kwenye uponyaji wa vizazi. Njia ya kuusema ukweli itachukua nafasi kwenye kupitia taifa kumulika mwanga kwenye makosa ambayo yalifanyika dhidi ya mwanyarwanda. Hii itasahihisha kwa mara ya kwanza, haki ya ushindi ya RPF kwenye mahakama ya Gacaca na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai ya Rwanda ambayo haikupeleleza makosa yaliyofanywa dhidi ya wahutu.

- Kuwaachia wafungwa wote wa kisiasa pasipo masharti, wale waliofungwa kwenye nyumba za siri, utangazwe hadharani na rasmi msamaha kwa wafungwa wote ipisokuwa kwa wale wahalifu wakubwa pamoja na waanzilishi na waendeshaji wa mauaji ya kimbari.
- Wanyarwanda kutambua ya kuwa yalikuwepo mauaji ya kimbari dhidi ya wahutu na watusi.
- Dunia itambue mauaji ya kimbari dhidi ya wahutu na kuwaleta mbele ya haki wale wote waliohusika kuandaa na kusimamia mauaji hayo

- Kupitisha uchunguzi juu ya nani alifanya mauaji ya Rais Juvenal Habyarimana na Rais Ntaryamira wa Burundi na wote waliokuwa kwenye msafara wao siku ya tarehe 6 Aprili, 1994. Wahusika wote waletwe mbele ya vyombo vya haki.
- Kutengeneza na kimarisha orodha toshelezi ya wahanga wa watusi na wahutu katika **Kitabu Cheusi cha Kumbukizi**
- Uwepo wa wizara mpya ya wahanga wa mauaji ya kimbari
- Ondoa mabaki yote ya miili yaliyoko kwenye maonyesho ya wazi kwenye makumbusho na kuyahifadhi kwa heshima istahiliyo.
- Tenga kilima kimoja kama Kilima **cha Kumbukizi** ambapo **Makumbusho ya Mauaji ya Kimbari** na **Makumbusho ya Historia ya Rwanda** itajengwa. Makumbusho ya Mauaji ya Kimbari yatakuwa pamoja na mambo mengine, majina ya wahanga wote wa mauaji hayo.
- Kutengwa kwa siku moja maalumu ya taifa kama **Siku ya Kumbukizi**
- Kifanye Kitabu Cheusi cha Kumbukizi kiwe sehemu ya nyaraka ya nyongeza kwenye katiba ya Rwanda ambayo kila mwananchi lazima ailinde na kuiheshimu na ambacho kitakuwa mojawapo ya vitabu vitumikavyo kula viapo kwa nchi.
- Uundwe mtaala mpya wa elimu ya **Historia ya Rwanda** kwa ajili ya shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati vya mafunzo ambavyo hutilia maanani alama za masilahi jumuishi ya kijamii, kisiasa na kitamadui.
- Jadili muafaka wa kitaifa juu ya alama mpya za taifa kwa kujumuisha Wimbo wa Taifa na Bendera ya Taifa
- Chunguza na tafiti mazingira na maeneo hasa ambapo wahanga wa mauaji ya 1973 walizikwa ili hatimaye familia zao ziweze kutambua na kuwapa mazishi stahiki.
- Rudisha mabaki ya mfalme Yuhi Musinga, na Rais Juvenali Habyarimana kwa ajili ya mazishi nchini Rwanda
- Utafiti wenye kamisheni uangalie kwenye mauaji ya kimkakati dhidi ya watusi mara baada ya mapinduzi ya kihutu ya 1959
- Mazungumzo yaanze juu ya **“Kupona Pamoja”** nchini Rwanda baina ya wakimbizi na wale wa ughaibuni.
- Iundwe Tume ya Taifa Maalumu ili kushughulika na hali ya Twa

5. *Ubunifu wa kijamii na kiuchumi*

Kama ilivyotajwa hapo awali, idadi ya watu nchini Rwanda inakadiriwa kuwa maradufu mpaka milioni 23 miaka 30 kutoka sasa (2050) na kufikia milioni 33 ifikapo 2100. Wastani wa kuishi wa

mtoto anayezaliwa leo Rwanda yaweza kuwa zaidi ya miaka 80. Kwa kutazama baada ya mtoto kuzaliwa inatafsirika kwenye kufikiri kuhusu hali yake wakati wa kuzaliwa. kiwango cha uchumi jamii wa familia, jamii ambamo mtoto atakulia, elimu atakayoipata, mazingira ya kazi, mtandao wake kwenye jamii, kuelekea kwenye utu uzima na kustaafu ndani ya miongo saba ijayo.

Ifikapo mwaka 2100, kuna uwezekano mkubwa wakulima wa chini wa Rwanda wenye uchumi wa chini hawatakuwepo tena. Kila uamuzi tuufanyao leo ni kuchagua kati ya kuijenga kesho yenye amani na usalama kwa wanyarwanda wazaliwao, kundi kubwa la wakulima maskini waishio vijijini au kuwatumbukiza kwenye maisha mafupi na ya dhiki.

Shughuli za leo na kesho za kisiasa, kijamii na hata kibiashara inabidi ziwe katika mlengo wa kulea, kujenga na kulinda kila kizazi ili kiishi maisha ya uhuru, ukamilifu, afya njema na faida. Hatimaye zile njia za kisiasa, kijamii, uzalishaji na matumizi zilizotumiwa na wafalme wa Rwanda zilifikia ukomo. Kwa kiwango fulani uvamizi wa kikoloni, uporaji na umiliki wa jamii nzima uliipatia Rwanda jaribio hatarishi la kisiasa mara baada ya ukoloni. Wakati utawala binafsi unatolewa sasa, yamekuwepo maboresho ya kiasi katika hali ya asilimia ndogo ya wanyarwanda kwenye kila enzi zilizofuatana, maisha ya wakulima maskini yamebaki kuwa mafupi na hatarishi.

Tunajifunza kutokana na historia yetu na mienendo mizuri na mibaya ya jamii nyinginezo kwenye historia ya ulimwengu. Kwa kuwa Rwanda ilijipatia uhuru wake mwaka 1962, zipo nchi nyinginezo nje ya Afrika ambazo zimehitimu kutoka kwenye hali ya kuwa nchi maskini kwenda kwenye hali ya kuwa nchi tajiri. Jamii kama hizo zimeweza kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye afya, sayansi, hesabu, teknolojia, uwezo wa kufanya biashara, utamaduni wa kuweka akiba, kodi za wastani, sera za viwanda ambazo nchi husika ziliona ni faida kwa maendeleo yao.

Kwingineko, mataifa yenye nguvu za kiuchumi yalikuwa hivyo kwa sababu himaya zao kimsingi zilipora ulimwengu walioutawala (ukoloni wa Ulaya kwa Afrika) au/na kuwafanya watumwa watu wote (Marekani ilifanya watu weusi kuwa watumwa). Kutoka kuwa jamii zilizotegemea sana kilimo kwa kutumia zana za mikono, wamekuwa juu ya mstari wa maendeleo kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda. **Mapinduzi ya Kwanza ya Viwanda** (makaa ya mawe, maji na mvuke kati ya miaka ya 1700); **Mapinduzi ya Pili ya Viwanda** (ugunduzi wa umeme na uzalishaji wa kiwango cha juu kwenye miaka ya 1800); **Mapinduzi ya Tatu ya Viwanda** (mifumo ya kidigitali na kompyuta, transista, vichataka taarifa , roboti, mifumo ya otomatiki, mitandao, mawasiliano ya habari kutoka miaka ya 1950 na kuendelea); na mapinduzi ya sasa, **Mapinduzi ya Nne ya Viwanda** (mifumo ya kompyuta yenye kufikiri na kuamua kama binadamu, teknolojia ya kubadili vinasaba, mifumo ya uchambuzi wa takwmu za kibiolojia, nishati mbadala, uchapishaji wa picha za viwango vya ubora, magari yajiendeshayo na mitandao ya vitu mbalimbali. Ili kuwa matajiri endelevu, mataifa haya yamepigana vita vya makusudi na ya kikatili wenyewe kwa wenyewe, yametwaa milki ya nchi nyinginezo, yameharibu mazingira kwa

kiwango kikubwa mno na wakaazi wa asili, maujaji ya kimbari, wametengeneza usawa usio linganifu kwa kupitia mifumo hatari ya uzalishaji na matumizi. Ni lazima tuepuke njia hizi katika kutengeza uchumi.

Ndiyo maana, dunia ya wanyarwanda wazaliwao leo watakua mpaka 2050 na 2100 ni dunia ya changamoto nyingi sana na fursa changamshi. Tawala za Rwanda tangu 1962 zimefuata mfumo wa maendeleo uliopendekezwa na mataifa yenye nguvu za kiuchumi, mashirika yao jumuishi ya misaada, mashirika ya kimtaifa wanayoisimamia (Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa). Wanakopesha, wanapokea misaada, wanatengeneza madeni alafu wanaomba msamaha. Tawala za kimabavu, vibaraka ambao wanajikita katika kutumia badala ya kuwa wazalishaji wakubwa, wamewekeza kwenye uagizaji wa bidhaa nje au uagizaji mdogo wa mabadilishano au usafirishaji wa bidhaa nje ya jiji la Kigali huku wakipeleka watoto kusoma nje ya nchi na kutunza utajiri wao nje ya mipaka.

Jenerali Kagame kwa kiasi kikubwa amewapita watangulizi wake wote kwa kukana ukweli ya kuwa yeye ni kama kiongozi kamili wa kifalme atawalaye wakulima maskini waliyo chini yake. Hupendelea kujiweka kama mtendaji mkuu wa Mapinduzi ya Tatu na ya Nne ya Viwanda. Kwa kujilimbikizia utajiri, kumiliki magari, ndege, majumba makubwa ya kisasa, uagizaji wa ndege za droni na uendeshaji wa makampuni yasiyo tengeneza faida huku akitaka kuuaminisha umma wa wanyarwanda kuwa wao ni matajiri. Kama mtendaji mkuu wa shughuli za nchi tajiri, maraisi, mawaziri wakuu, benki ya dunia na watendaji wa shirika la fedha la kimataifa wamesifia, wamemfadhili na kumlinda kiasi cha kumfanya asiweze kuwajibika kwa makosa ya kikatili aliyoyafanya dhidi ya wanyarwanda na majirani zao, yeye anauamini uongo wake mwenyewe.

Kupitia nishati za kijasiriamali na ugunduzi, wanyarwanda waanze kuandaa mikakati ya kiuchumi na kijamii ambayo itakisaidia kizazi cha sasa na kijacho kuweza kuzitatua changamoto na kuzichangamkia fursa.

- Kuandaa utamaduni wetu kuelekea kwenye ubunifu wa kibiashara na kijamii kuanzia ngazi ya chini mpaka juu
- Uandaaji wa maarifa na ujuzi kwa ajili ya ujasiriamali na ubunifu kwa ajili ya uchumi wa kilimo vijijini
- Elimu bure kuanzia ngazi ya msingi, sekondari na vyuo vya kati
- Kujikita katika mafunzo hasa kwa kuhimiza sayansi, tekinolojia, uhandisi na hesabu
- Kujikita katika utoaji wa huduma za afya za msingi, afya ya jamii na afya ya umma
- Kubuni mifumo madhubuti ya ikolojia, utamaduni, taasisi, jamii yenye kusaidiana na kunia pamoja, miundombinu na taasisi za kifedha

- Kubadili muelekeo wa taasisi za elimu kwa ajili ya kuandaa na kutoa mafunzo endelevu yenye kutoa nafasi ya kufikiri kwa kina, elimu ya uraia, ustahimilivu, uhuru wa kujieleza, ujasiriamali na ubunifu.
- Kuifanya Rwanda kuwa kitovu cha dunia na kanda ya lugha mbalimbali
- Kubuni upya duka la pamoja ili kutoa huduma jumuishi na stahiki, ikijumuisha mitaji kwa biashara zenye mitaji midogo inayomilikiwa au kusimamiwa na wanawake, vijana, wanajeshi walioachishwa kazi na manusura wa mauaji ya kimbari
- Kujenga mfumo madhubuti na wa kina kwa ajili ya wazee na wale wasiojiweza
- Kujenga uwezo wa taifa na kanda kwa ajili ya biashara za kikanda na ki-umajumui wa Afrika kwa kuziona fursa zilizomo kwenye asili ya Afika Mashariki
- Kupitia ushirikiano na jamii ya kimataifa, kutafutwe na kurudisha utajiri wote ambao jenerali Kagame na washirika wake wa karibu wamewaibia watu wa Rwanda na Kongo. Utajiri huo utakaorejeshwa utumike kuwasaidia wajane, yatima, waliokatwa mikono, manusura wa mauaji ya kimbari na wanajeshi walioachishwa kazi.

6. *Kituliza nchi ya Rwanda ndani ya Jumui ya mataifa ya Afrika Mashariki*

Mnamo mwaka 2050, idadi ya watu jumuishi ya Tanzania (137 milioni), Uganda (100 milioni), Kenya (97 milioni), Burundi (25 milioni), Rwanda (24 milioni), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (200 milioni), Sudani ya kusini (20 milioni) itakuwa juu ya milioni 600. Ukijumlisha idadi ya watu wote katika mataifa haya sita ifikapo mwaka 2100 inakadiriwa kufikia watu milioni 1026. Kwa ufupi, ni wanajumuia wa Afika Mashariki bilioni 1. Na hawa ndiyo watabaki kuwa majirani wa Rwanda.

Mazuri na mabaya ya mnyarwanda mchanga au vijana wa sasa yatajengwa na changamoto na fursa zilizomo kwenye ukanda huu.

Kidunia, mazingira ya ukanda huu yatajengwa na majanga, migogoro, kuyumba kwa uchumi, teknolojia, ongezeko kubwa la vijana kukosa ajira, tishio la mifumo ya kimtandao, uharibifu wa mazingira uliokithiri, silaha kubwa za maangamizi, kuanguka kwa mataifa, kugombaniwa kwa maliasili, usambazwaji wa mihadarati, kuongezeka kwa mwanya kati ya wenye nacho na wasio nacho kijamii na kisiasa pamoja na ushindani wa kidunia.

Tunavozidi kuifikiria Rwanda mpya tunayoijenga itakavyokuwa, inabidi tupanue fikra zetu kwa namna ya kuikubali na kulikumbatia taifa kubwa. Inatubidi tuijenge pamoja na majirani zetu, wana taifa la Afrika Mashariki. Taifa hili jipya la wakazi milioni 600 mwaka 2050 au bilioni 1 ifikapo mwanzo mwa karne mpya litaundwa na wanchi wafanyao kazi kwa bidii pamoja na rasilimali nyingi sana. Hali hii itatengeneza fursa ambazo ndizo zitaleta mabadiliko makubwa.

Siyo tu mafanikio haya mapana ya muungano wa kijamii, kisiasa na kiuchumi yatawaweka salama watu wa Afrika Mashariki, yatetengeneza utambulisho mpya ambapo kuwa Mhutu, mtusi, mtwa, au hata mnyarwanda itakuwa sehemu ndogo tu ya uhalisia wenyewe. Jambo la msingi kabisa wanyarwanda, kama wananchi wa taifa la Afrika ya Mashariki wanaweza kuchagua kuishi popote pale kwenye hii jamii pana badala ya kuwadidimiza ili wajifungie kwenye vilima vya Rwanda. Juu ya yoye, makubaliano ya pamoja ya usalama baina ya nchi wanachama wa shirikisho hili la taifa la Afrika Mashariki litakuwa na rasilimali za kujitosheleza kulinda wananchi wao dhidi ya chokochoko za ndani na nje.

Lengo hili la kuwa na taifa la Afrika Mashariki halitaweza kufikiwa wakati utawala wa Jenerali Kagame utaendeleza uvaaji sura ya kivita ya kuzichokonoa nji jirani na mwendelezo wa utawala wa kiimla wa ndani ambao unalindwa na hofu inayojengwa na vikosi vya siri vya polisi. Utawala wa Rwanda unadai hadharani kuwa unaunga mkono jumuiya ya Afrika Mashariki lakini nyuma yake kwa siri unazorotesha na kuuhujumu kwa sababu jumuiya haitatii mbinu zake za kuifanya jumuiya hii iwe chini yake.

- Kuanzishwa kwa mijadala ya uponyaji na mapatano na wananchi wa Afika Mashariki pamoja na serikali zake
- Kuanzishwa kwa kwa mijadala ya uponyaji na mapatano na serikali na watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
- Ziwepo jitihada za kidiplomasia ili kuendeleza mabadiliko ya taifa la Afika Mashariki
- Kuanzishwa kwa mikutano mikubwa ya kila mwaka itakayokuwa inaendeshwa na wananchi wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kuunda muundo wa namna taifa linavyopaswa kuwa
- Kuunda mtandao shirikishi baina ya vyuo vya umma na binafsi ndani ya Afrika Mashariki ili kuweka wazi na kuhalalisha ni kwa namna gani watawawezesha wananchi kwenye amendeleo ya dhana nzima ya mabadiliko salama ya tabia ya nchi kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda.

7. *Majadiliano Mapana: Majadiliano ya mkataba wa jamii itakavyoishi.*

Ijapokuwa mafanikio makubwa kwenye utawala wa Rwanda umeweza kuweka mazingira ya upigaji kura, mifumo ya sheria na kikatiba, lakini haya hayakuwa matunda ya muafaka wa kitaifa, mwishowe yakageuka kuwa ya muda mfupi. Mshindi katika ushindani wa siasa za mabavu baina ya watu mashuhuri wa koo unaeleza kwa kiasi gani katiba hiyo, sheria na maandalizi ya uchaguzi yanahalalisha utawala wake.

Kwa mabdiliko ya utawala, nguvu ya watawala unapingana na makubaliano ya nyuma na kutengeneza makubaliano yao. Ambapo serikali haijaanzishwa kwa matakwa ya wananchi,

hawajaona inafaa kutafuta uthibitisho wa wananchi wake katika kuunda misingi thabiti ambayo ndiyo inapaswa kusimamia kanuni, tamaduni, maadili na taasisi za jamii husika kwa ajili ya maslahi ya pamoja.

Katiba na sheria hutengenezwa kwa kutazama matakwa ya sasa, kwa jicho la kukumbuka yaliyopita na maono ya yale yajayo. Kama historia ya Rwanda katika karne iliyopita imekuwa ya kugombania madaraka kwenye mahakama ya mfalme, utawala wa kikoloni, mabadiliko ya tawala za kimabavu, mapigano baina ya makabila na koo, mauaji ya kimbali, vita ya wenyewe kwa wenyewe, umaskini, utawala wa kiimla, ni aina gani ya mtazamo wa kibinadamu ulijadili makubaliano ya jamii itakavyoishi kama tunataka kuzikabili hatari hizi kubwa kuwahi kutokea? Kama nia yetu ni kuwa na katiba na sheria ambazo zitaikabili karne hii na ile ijayo katika uhalisia wa Afika Mashariki na ulimwengu kwa ujumla, ni maandalizi gani thabiti tunayafanya leo?

Kipindi cha migogoro ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, wakati na wa hitaji la majadiliano ndilo hitaji kuu sana, wasomi wa Rwanda wamechagua kubakia na mipango yao yenye ubinafsi. Wafalme wa Rwanda hawakuwahi kuhitahi idhini ya wataliwa. Hata watawala wa kikoloni hawakuhitaji idhini ya watawaliwa wao.

Wakati ikielekea kwenye mapinduzi ya wahutu ya mwaka 1959, fursa ndogo ya majadiliano kwa ajili ya kesho ya Rwanda ilijitokeza kwa watawala wa kifalme. Lilikuwa kundi dogo lakini lenye kupiga hatua la kihutu likipigania ukombozi wa wingi wa jamii ya kihutu. Mwezi wa Tano mwaka 1958, washauri wakuu wa Mfalme Mutara Rudahigwa wa watusi, waliandika waraka ambao ndani yake walijenga hoja ya kuwa haitakuwepo kwa msingi wowote wa udugu kati ya wahutu na watusi. Walisema ya kuwa, tangu wahutu watawaliwe wamefanywa kuwa watumwa.

Mnamo tarehe 27 mwaka 1959, hali ya ukinzani iliongezeka, Gregorie Kayibanda aliandaa ombi lenye hisia za ubaguzi wa wahutu na watusi kwenye makundi mawili tengano. Raisi aliyekuja aliwaelezea wahutu na watusi kama nchi mbili ndani ya taifa moja, nchi mbili ambamo kati yao hakuna mawasiliano, mshikamano, wanaopuuziana tabia zilizomo baina yao, fikra na hisia kana kwamba wanaishi katika kanda tofauti, viumbe wa sayari tofauti.

Mabadiliko ya historia, utawala wa kikoloni, kanisa Katoliki, ibada za wahutu vyote vilikuwa kwenye upande wa kihutu ambao wakati huo waliamua yale yaliyomomo kwenye mfumo wa sharia na katiba. Mfalme na watu mashuhuri wa watusi wakabaki hstoria.

Ndani ya miaka kumi ya tangu Rwanda ijipatie uhuru kutka kwa Ubelgiji, watu mashuhuri wa kihutu hawakukubalina baina yao hivyo kupelekea kwa mapinduzi ya kijeshi yaliyoongozwa na wahutu wa Kaskazini ambayo yalimuweka madarakani jenerali Habyarimana. Watu mashuhuri waliokuwa sehemu muhimu ya mapinduzi kihutu ya mwaka 1959 walifutiliwa mbali.

Vita ya wenyewe kwa wenyewe ya waasi wa kitusi dhidi ya serikali ya kihutu yaliibuka mwaka 1990, fursa nyingine ilijitokeza kwa ajili ya majadiliano ya makubaliano mapya ya kisiasa, kisheria na kikatiba kwenye mchakato wa amani wa Arusha.

Watusi na wahutu walioingia vita hiyo mara moja waliuita mchakato huu kuwa ni wa kugawana madaraka. Kiukweli, haikuwahi kujadiliwa akilini mwa wanyarwanda. Ilikuwa kama kugawana mabaki baina ya mahasimu katika mchakato batili wa kugawana madaraka. Kwa shingo upande, pande zote mbili zilitia saini makubaliano ya kule ya Arusha mwezi Agosti 1993, kila upande uliendelea kujiandaa kwa mtifuano wa mwisho ulioanza tarehe 6 mwezi Aprili mwaka 1994. Mara baada ya kumuua mtia saini mwingine wa Mkataba wa Arusha wa Amani na kukomesha mapigano ya silaha, jenerali Kagame pamoja na kundi la wafuasi wake wa kitusi harakaharaka wakahitimisha mapigano ya kijeshi ndani ya siku 100 ambayo yalihitimishwa na kile walichokiita jaribio la utawala wa kihutu uliodumu muda mfupi.

Hivyobasi, historia ya Rwanda haina majadiliano makusudi ya mkataba wa namna gani jamii iishi ulioainishwa kwenye makubaliano, na mfumo wa upigaji kura, kisheria na kikatiba unayolinda maslahi mapana ya wanyarwanda.

Bado yapo mengi ya kuongelea miongoni mwetu kadiri tunavyofanya majadiliano shirikishi na stahimilivu ya mfumo wa jamii inavyopaswa kuishi kwa ajili ya kizazi hiki na vile vijavyo. Jenerali Kagame na vikosi vya siri vya polisi wamekuwa wapinzani na vikwazo vya kupiga hatua kwenye nchi yetu. Lazima tuendeleze majadiliano haya muhimu huku tukijua fika ya kuwa atayapinga kwa kutumia nguvu na mabavu aliyonayo mpaka pale atakapo tupiliwa mbali ili akaungane na watawala wa mabavu wenzake huko kwenye jalala la historia.

Lazima tuwe wakweli baina yetu na tuuseme ukweli kwa wale walioko madarakani na kwetu sisi wenyewe. Kwa sasa wanyarwanda wapo kwenye umaskini na wapo kwenye hali ya huzuni mno. Wanyarwanda hawajaweza kuvishinda visababishi vya vita ya wenyewe kwa wenyewe, mauaji ya kimbari, mizozo baina ya makabila na koo, mgawanyiko pamoja na ongezeko la mwanya wa wasio nacho na wali nacho. Rwanda haijapata uponyaji wa simanzi isiyoisha. Rwanda haitawaliki. Kumaliza tofauti zilizopo kumebaki kuwa tumaini la mbali. Utajiri wa chi umebakia mdogo na mara nyingi ukifungamanishwa na jenerali Kagame, familia yake na baadhi ya watusi wachache wanaomzunguka. Nchi ya Rwanda haiwajibiki kwa wananchi wake. Maamuzi na utungaji sera nchini Rwanda siyo wa kidemokrasia, bali kidikteta. Jenerali Kagame na bunge hawachaguliwi katika uchaguzi huru na wa haki. Hakuna mfumo wa udhibiti baina ya mihimili ya serikali, bunge namahakama. Rwanda inatwaliwa pasipo utawala wa sheria. Uhalifu uliofanywa na utawala wa Kagame dhidi ya jamii ya wahutu haitambuliki na wala wahusika kuwajibishwa. Jamii ya wahutu hawana idadi ya waliopoteza maisha. Hakuna uhuru wa asasi za kiraia. Hakuna

uhuru wa kujieleza wala uhuru kupata habari. Wanyarwanda wengi wanaishi katika hali ya hofu asiyoisha, vitisho na tishio la kifo.

Wanyarwanda wanapaswa kujadili mkataba wa namna ya jamii kuishi, ili wayakabili haya yote, na wayafanye haya kwa mara ya kwanza.

WITO WA YA DHARURA.

Kwa muda mrefu vilima vya nchi ya Rwanda vimekuwa maeneo ya uhalifu. Damu ya kupita kiasi imemwagwa kwenye vilima hivi, mabonde, kona na pembe ya hii nchi vumilivu. Ardhi yetu imeharibiwa mno kwa matendo ya vibaraka wenye njaa na vurugu ambao wameigeuza Rwanda kuwa kaburi kubwa kupitiliza. Hakuna familia hata moja Rwanda, zikiwemo familia za vibaraka ambao wameiacha nchi yetu patupu wameepushwa na simanzi, huzuni na majonzi. Kupitia matendo yetu, tofauti zote na ukimwa wetu tumechangia huu uwendawazimu, machafuko na kuharibikiwa huku ambako kumeharibu jamii ya Rwanda kizazi na kizazi.

Vilima hivi vya damu vilivyobakia na huzuni, utupu, simazi na machozi vitageuzwaje kuwa vilima vyenye kuponya? Nani atauguza vidonda vya yatima, wajane, manusura wa mauaji ya kimbari na maskini? Ni nani atakomesha ukandamizaji, kutengwa na chuki itufanyayo tuwe jeuri? Tunaweza kufanya vyema zaidi ya vile?

Yatupasa wanyarwanda kutoutafuta muujiza nje yetu sisi. Ni lazima tutazame ndani yetu. Hapo ndipo suluhishi lilipo, kwenye fikra na matendo yetu. Lazima kuukabili ukandamizaji unaotuzuia kutambua ya kuwa sisi sote ni sehemu ya mwili mmoja au familia moja iitwayo Rwanda. Pale eneo moja la mwili linapoumwa, mwili wote unajeruhiwa. Hii ni shughuli ya mioyo na fikra zetu. Kwa kutambua kuwa tu jamii inayoumwa, lazima tukatae na kugomea mizizi ya majonzi. Hatuhitaji fedha, watu kutoka nje au idhini ya wale watusababishiao huzuni ili kuweza kuponya vidonda vyetu na kutibu majeraha ya wenzetu.

Ni lazima na tutajikomboa wenyewe kutoka kwenye ukandamizaji.

Tutalileta pamoja na kuliponya taifa letu.

Tutajipa nguvu wenyewe kwa wenyewe ili kutengeneza taifa endelevu na thabiti ambalo watu wake, familia na jamii kwa ujumla hushamiri.

Tutaunda upya taifa la Afrika Mashariki lenye usalama wa kutosha na lenye kufanikiwa.

Ni lazima kuanza leo, siyo kesho.

Washington, D.C.

Marekani Mei 30, 2021

Mawasiliano:

Dr. Theogene Rudasingwa Barua pepe: ngombwa@gmail.com

Sixbert Musangamfura Barua pepe: sixbert.musangamfura@gmail.com